# Nipashe Jumapili

Jumapili Januari 14, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581555

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Tanzania** 10 bora Afrika kwa madeni kiduchu



UKURASA 3

**Meneja** TANROADS aliyefariki katika riadha aagwa, kuzikwa Kahama

UK. 4



**4R** za Rais Samia zinavyowaweka Watanzania pamoja

UKURASA 8



NGOZI BILA MICHIRIZI

UKURASA 14



# CHADEMA 'yaitia tembo maji' miswada sheria uchaguzi

UKURASA 2

Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kufanya maandamano kupinga miswada ya sheria iliyowasilishwa bungeni yanayotarajiwa kuanza Januari 24 mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watu 18 wafa kwa kufukiwa na kifusi mgodini

UKURASA 4

# Trafiki afariki kwa kugongwa na daladala



UKURASA 3

**MICHEZO** GAMONDI KUCHUKUA UAMUZI MZITO YANGA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Ndugu wa aliyepigwa risasi watishia kuishtaki TFC

**Na Beatrice Shayo**

MVUTANO ulioibuka juzi Tegeta Machinjioni, Dar es Salaam, kati ya askari sita wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na vijana wanne na kusababisha asiyehusika kujeruhiwa kwa risasi, umechukua sura mpya baada ya ndugu kutishia kufungua kesi dhidi ya wakala huo.

Katika mvutano huo, askari hao wa TFS inadaiwa walikuwa wakifukuzana na wafanyabiashara wa mkaa na katika purukushani za kuwakamata, ndipo risasi zilitumika na kumjeruhi eneo la kichwani, Samson Lugendo (26), ambaye ni muuza nyama (bucha).

Majeruhi mwingine ni askari wa TFS aliyekuwa na silaha ambaye ambaye katika harakati za kuwasaka wafanyabiashara wa mkaa, alidondoka na kukatwa panga mgongoni na mmoja wa watuhumiwa hao, kisha kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kaka wa majeruhi huyo, Zabron Lugendo (30), akizungumza na Nipashe juzi kwa njia ya simu baada ya ndugu yao kuruhusiwa kutoka katika Hospitali ya Kitengule, alisema mpaka wakati huo hakuna mtu yeyote wa TFS aliyejitokeza.

"Tunakusudia kufungua kesi dhidi ya TFS kwa sababu wao ndio waliomjeruhi ndugu yetu, lakini hawajajitokeza. "Hospitali wametuambia gharama za matibabu zinaishia leo (jana) kama kutakuwa na changamoto ya mgonjwa gharama zitatuhusu ndugu," alisimulia.

**HALI YA MGONJWA**

Lugendo alisema mdogo wake aliruhusiwa kutoka hospitalini juzi ingawa bado analalamika ana maumivu.

"Mgonjwa bado analalamika anajisikia vibaya, anapata maumivu makali kichwani na hospitali imemruhusu kuondoka," alisema.

Kuhusu gharama za matibabu yake, Lugendo alisema zimelipwa ingawa hawajajua ni nani aliyefanya malipo hayo.

"Tumeambiwa gharama zimelipwa, ila kujua ni nani amelipa, hawajataka kutuambia," alisema kaka wa majeruhi.

Lugendo alisema jeraha alilolipata ndugu yake ni kubwa kutokana na risasi kumpitia na kuchana fuvu, hivyo ameshonwa nyuzi zaidi ya 10.

Alisema kikubwa wanachokitaka kutoka kwa serikali ni kupatiwa haki ya mdogo wake kama fidia kutokana na majeraha aliyoyapata katika mwili wake. Pia alisema kijana huyo ni mtu anayetegemewa na familia yake na kwa sasa yuko kitandani anauguza jeraha, huku yeye (kaka) akiendelea kumhudumia.

"Tunaiomba serikali iingilie kati ili tuweze kujua muafaka wa hili jambo. Jana tumefuatilia kituo cha polisi wakatuambia tuondoke bado hawajamaliza kufanya upelelezi na kesi, bado haijakabidhiwa kwa mpelelezi.

"Sisi tulienda kufungua kesi ya kudai fidia kwa mtu ambaye alimsababishia majeraha, hatujajua ni kiasi gani, tulitaka kujua sheria inaeleza ni kiasi gani mtu anatakiwa kupewa fidia ambaye amepata majeraha hayo," alisema.

Hata hivyo, Lugendo alisema waliofanya tukio hilo kama wapo tayari kufanya mazungumzo na familia nje ya polisi wako tayari na kwamba wameamua kukimbilia kudai fidia kwa sababu, hata matibabu yenyewe wamefanya kutumia nguvu kubwa kwa kuwa, hawapati ushirikiano kutoka upande wa pili.

"Tangu mdogo wangu amepata jeraha juzi, hatujapata upande wa pili ambao ni TFS kujua hali ya mgonjwa wao, hadi muda huu hatuna taarifa zao, licha ya kuruhusiwa kutoka hospitalini," alisema.

Lugendo alisema hawana fedha ya kuendelea kumuuguza mgonjwa wao, kwani taarifa kutoka hospitalini wameambiwa matibabu ya mgonjwa yameishia jana, na hali yake ipo vizuri licha ya kwamba bado ana maumivu.

"Madaktari wametuambia tunatakiwa kurudi nyumbani matibabu wamemaliza, wamemuona mgonjwa amepona, lakini analalamikia bado kichwa kinamuuma ila tunashindwa kuelewa, huyu atatakiwa kwenda kuripoti hospitalini kwa ajili ya kusafisha kidonda au la,"alisema Lugendo.

Alisema walijua mgonjwa wao wataendelea kumpeleka hospitalini hapo kwa ajili ya kuendelea kutibu jeraha hilo, lakini hospitali imewajulisha gharama za matibabu zimeishia jana na endapo wakihitaji zaidi watatakiwa kulipia.



Mwenyekiti wa kijiji cha Mikwamba, wilayani Muheza mkoani Tanga, Ceca Nyoka akizungumza katika mkutano wa hadhara uliojadili ujenzi wa shule mpya ya msingi ya darasa la awali na la kwanza, kijijini hapo juzi. Kulia ni Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Rose Mfaki na Polisi Kata ya Magila, Frank Mwemsi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# CHADEMA 'yatia tembo maji' miswada sheria za uchaguzi

**Na Beatrice Shayo**

MGEMA akisifiwa tembo hulitia maji. Msemo huo unasadifu na hatua iliyofikiwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutokana na msimamo kilioweka kuhusu miswada ya sheria kuhusu masuala ya siasa na uchaguzi, iliyowasilishwa bungeni.

Wakati wadau mbalimbali wakiendelea kutoa maoni kuhusu miswada hiyo, CHADEMA kimetangaza kufanya maandamano ya amani nchi nzima kushinikiza kuondolewa bungeni.

Pamoja na msimamo huo na tishio la kufanya maandamano, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, alipoulizwa, alisema wamesikia lakini ni mapema kusema au kutoa tamko lolote.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alitangaza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi mpya za chama hicho, Mikocheni, Dar es Salaam akibainisha kwamba uamuzi huo unatokana na maazimio ya kikao cha dharura cha Kamati Kuu kilichofanyika Januari 8, mwaka huu.

Wakati Mbowe akitoa uamuzi huo, Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilikamilisha muswada iliyosomwa bungeni Novemba, mwaka jana, kuhusu miswada minne.

Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023, Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa mwaka 2023.

Mbowe alisema CHADEMA inayakubali maridhiano lakini yamekiukwa, hivyo wanakusudia kufanya maandamano nchi nzima kwa kuanza na mkoa wa Dar es Salaam, Januari 24, mwaka huu. Alisema maandamano hayo ya amani yanalenga kuishinikiza serikali kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa uchaguzi.

"Kwenye suala la maridhiano ni kweli nilimwamini Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu alilitangazia taifa, aliruhusu mikutano ya hadhara na alisema yuko tayari hata kuupoteza urais wake lakini alete mageuzi makubwa katika nchi yake.

"Leo ninasema simwamini na chama chake kwa sababu miswada yake, haiakisi R4 anazozihubiri yeye na wenzake. Kiongozi anapaswa kutembea katika maneno yake anayoyatoa, na maneno yake hayapimwi kila siku, yanapimwa kwa wakati," alisema.

."Mazingira yaliyokuwapo mwaka jana sio yaliyokuwa mwaka huu, mimi binafsi niliamini kwa sababu niliongoza mazungumzo yale, na unapokaa na watu wazima wakakubali, kwa nini nisiwaamini," alihoji na kuongeza;

"Tusubiri kuiona miswada itakapotoka, tuone ina akisi kile tulichozungumza. Kilichotokea hayakupuuzwa ya CHADEMA peke yake, bali pia ya waangalizi wa kimataifa yamepuuzwa na wadau wengine.

Mbowe alisema viongozi walijitokeza na kuahidi kurekebisha yale yaliyojitokeza katika uchaguzi uliopita na walikiri kuwapo na mapungufu, lakini matokeo yake maoni yaliyowasilishwa hayapo kwenye miswada licha ya kuwasilisha.

"Chama ni chama kinachosikiliza neno la kujitoa ama kutokujitoa halina mantiki katika kikao chetu tunachokwenda kuandamana, lakini chama hiki hakitaacha kuamini katika maridhiano kwa sababu maridhiano muungwana ni binadamu. Kuamini katika maridhiano ni falsafa ya CHADEMA," alisema Mbowe.

Alisema kinachofanya kuandamana ni kutokana na wenzao wanayapuuza maridhiano na kuwa yakijitokeza mazingira ambayo yanaonyesha wamesikia kilio cha watu na kuyatekeleza hicho ndio wanachokipigania.

"Huko nyuma tulichagua kukaa kimya na kuwa wapole tukiamini kuwa upole wetu, ustaarabu wetu na uungwana wetu utawafanya wenzetu waone. Matokeo yake wametudhihirishia pasipo na shaka kwamba, hawapo tayari acha tutumie nguvu nyingine huenda watakuwa tayari huko mbele ya safari, maandamano ni lazima kufanyika,"alisisitiza.

Mbowe alisema maridhiano sio kwamba yamegharimu CHADEMA, yamewafanya wawe wakomavu katika siasa na lengo lao ni kuhakikisha wananchi wanapata haki zao.

Alisema CHADEMA ilifanya vikao vya maridhiano na serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuwasilisha mapendekezo ya namna ya kukwamua mkwamo uliopo katika eneo la Katiba Mpya, kuboresha mifumo ya uchaguzi na upatikanaji wa Tume Huru ya Uchaguzi.

Alisema wamejiridhisha hakuna maboresho yanayofanyika katika miswada hiyo na matokeo yake wanaita watu kwenye vikao na makongamano ili kuionyesha dunia kuwa, Tanzania inajadili maboresho ya miswada.

# Trafiki afariki kwa kugongwa na daladala

**Na Beatrice Shayo**

ASKARI wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Kituo cha Polisi cha Chang'ombe, Temeke mkoani Dar es Salaam, Koplo Glory Peter, amefariki dunia baada ya kugongwa na daladala akiwa kazini eneo la Mtoni Mtongani.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliliambia gazeti hili jana kuwa askari huyo alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke.

Alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 4:00 asubuhi Mtoni Mtongani mbele ya kituo cha mafuta cha Total, kilichoko barabara ya Kilwa, wilayani humo.

Trafiki huyo, alisema aligongwa na gari lenye namba za usajili T 558 DYY Nissan Civilian, ambalo dereva wake hajafahamika kutokana na kukimbia na kuliacha eneo la tukio.

"Daladala hiyo ilikuwa ikitokea Kwa Aziz Ally kwenda Mbagala. Ilipofika maeneo hayo, iliacha njia na kumgonga askari huyo aliyekuwa kazini pembeni mwa barabara," alisema Kamanda Muliro.

Alisema askari huyo ambaye alipata majeraha makubwa, alifariki dunia muda mfupi wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Temeke.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta dereva wa gari hilo ambalo kwa sasa liko kituo cha polisi.

Taarifa kutoka katika familia ya trafiki huyo, ilisema ndugu yao anatarajia kuzikwa kesho katika makaburi ya familia ya mume wake, Chanika jijini Dar es Salaam. Ameacha watoto wawili.




Mtu au watu wasiojulikana wakiwa wamepanda mti kwenye mashimo yaliyopo kwenye barabara ya Bibi Titi Mohamed, eneo la Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar es Salaam jana, kama ishara ya kuikumbusha Mamlaka husika, kuikarabati barabara hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania 10 bora Afrika madeni kiduchu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Kimataifa la Fedha (IMF) limeisifu Tanzania kuwa moja ya nchi 10 za Afrika zenye kiwango kidogo cha madeni hali inayoifanya iendelee kuaminiwa na kukopesheka na taasisi za kifedha za kimataifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na IMF na kukaririwa na jarida la Buisiness Day la Nigeria, Tanzania ina asilimia 41.8 ya madeni kulinganisha na uwiano wa pato ghafi.

"Taifa hilo la Afrika Mashariki kwa kiwango hicho kidogo cha uwiano wa deni na ukuaji uchumi unaonyesha kuendelea kuaminika, hivyo kuchangia ukuaji wa Uchumi na ustahimilivu," ilisema taarifa hiyo.

Nigeria inashika nafasi ya tisa katika kundi hilo la nchi za Afrika ambazo madeni yake ni himilivu kwa kuwa na asilimia 41.3. sababu kubwa ya kuwa katika hali hiyo ni kutokana na sekta mbalimbali za kiuchumi na jitihada zinazochukuliwa katika ulipaji wa madeni.

Cameroon inashika nafasi ya saba ikiwa na asilimia 39.6 kutokana na kuweka mikakati madhubuti na nidhamu katika usimamizi wa fedha.

"Pamoja na kupambana na vikundi vya uhalifu na matatizo ya kiuchumi, Cameroon imeendelea kuwa makini katika udhibiti wa matumizi ya serikali. Kuendelea kusimamia mapato ya mafuta, rasilimali ambayo ni muhimu, kumeongeza uimara wa bajeti," taarifa hiyo ilibainisha.

Chad ambayo kwa muda mrefu imekuwa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, ni moja ya nchi ambazo bado uchumi wake umekuwa wa kuridhisha baada ya kurejea kwa kasi na kuwa na asilimia 38.7.

Hatua hiyo inatokana na kusuimamia kikamilifu mipango yake ya kifedha. Sababi zingine ni mkakati wa kupunguza madeni na uwazi katika usimamizi wa rasilimali.

Visiwa vya Comoro vina asilimia 36.9 katika orodha ya nchi hizo zenyev kiwango kidogo cha maden. Sababu kubwa za uhimilifu huo ni umakini katika matumizi ya mikopo, usimamizi mzuri na udhibiti wa bajeti.

Nchi zingine katika kundi hilo na asilimia kwenye mabano ni Equatorial Guinea (33.7), Guinea (31.5), Ethiopia (31.2), Botswana (18.1) na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (11.1),

# Abiria waliokwama wasafiri kwa mabasi

**Na Christina Haule,** Morogoro

ZAIDI ya abiria 1,200 waliokwama na treni ya reli ya kati katika kituo cha reli mkoani Morogoro, wamesafirishwa kwa mabasi hadi mkoani Dodoma na baadaye kusafiri kwa treni kwenda mikoani kwao.

Kaimu Mkuu wa Kituo cha Reli Morogoro, Herman Ngonyani, alisema jana kuwa abiria hao walisafirishwa juzi jioni kuanzia saa 1:30 na basi la mwisho liliondoka saa 4:15 usiku.

Ngonyani alisema mabasi hayo yalifika kituoni hapo yakiwa na abiria wengine waliokwama mkoani Dodoma ambao nao walipanda treni iliyogeuza baada ya kushindwa kwenda Dodoma na kwenda jijini Dar es Salaam.

Alisema abiria wa treni waliotoka mkoani Morogoro pia walifikishwa Dodoma kwa mabasi na usiku huo huo walipanda treni iliyokwama hapo na kugeuza kwenda mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma.

Kutokana na adha iliyojitokeza, Ngonyani aliwaomba wasafiri kuwa watulivu wanapopata changamoto zozote za usafiri hasa katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha nchini ambazo zinasababisha athari si kwa njia ya treni pekee bali hata kwa miundombinu ya barabara.

Katika hatua nyingine, mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali mkoani hapa zimesababisha nyumba 21 katika kata ya Dakawa, Mvomero mkoani hapa kuanguka na kusababisha watu kukosa makazi kwa sababu ya mafuriko yaliyotokea.

Diwani wa Dakawa, Yusuph Makunja, alisema jana kuwa wakazi hao wametoka katika vijiji mbalimbali katika vitongoji tisa vya kata hiyo ambazo zilijengwa kwa ujenzi wa kawaida usioweza kuvumilia maji.

"Nyumba zilizopata athari na kudondoka kabisa ni 21 zilizojengwa kwa ujenzi usiostahimili maji. Kila kitongoji utakuta nyumba mbili au tatu zimeanguka. Juhudi za kuwasaidia zinaendelea" alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, alilazimika kuwasaidia makazi katika Shule ya Msingi Dakawa huku akiwahimiza wakazi wa nyumba zingine kutoka kwenye nyumba zao wanapohisi wanaweza kukutwa na adha yoyote itakayotishia uhai wao.

Pia alisema wanaangalia namna ya kuwasaidia kwa chakula huku akiomba watu na taasisi mbalimbali kutoa misaada kwa watu hao.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...03/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ABDALLAH NDAKI ABDALLAH wa CHAMWINO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA AMINA MOHAMED KAMBI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 16 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 01 mwaka 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...02/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: EVA NDAMBO MBUGUYU wa TEGETA-DAR ES SALAAM**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MAJUTO ATHUMANI MBUGUYU**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 16 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 01 mwaka 2024

**HAKIMU**

## Watu 18 wafariki dunia kwa kufukiwa na kifusi mgodini

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

WATU 18 wamefariki dunia baada ya kufukiwa na udongo katika machimbo ya dhahabu yaliyopo katika kijiji cha Ikinabushu, Bariadi mkoani Simiyu.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Simiyu, Faustine Mtitu, alithibitisha jana kutokea kwa vifo hivyo huku akisema takribani watu 20 wanasadikika kuwamo ndani ya mashimo ya machimbo hayo.

Kamanda Mtitu alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 11:00 alfajiri na kwamba shughuli za uokoaji zilianza majira ya saa 12:00 asubuhi.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni kuporomoka kwa udongo kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha mkoani hapa ambazo zimesababisha mashimo hayo kuporomoka na kuwafukia wachimbaji hao.

Kamanda Mtitu alisema ukoaji umefanyika kwa kushirikiana na vyombo vya usalama vya mkoa huo na kwamba hadi saa 11:50 jioni miili hiyo 18 ilikuwa imeopolewa na kusitisha kazi hiyo kwa muda kutokana na giza kuingia na kwamba itaendelea leo asubuhi.

Miili hiyo 18 iliyoopolewa, alisema imehifadhiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Somanda na kwamba majina bado hayajatambuliwa kutokana na wakati wanaingia kwenye maduara hayo, hawakujiandikisha kwenye daftari.

## Watoto shule awali watembea kilometa tatu kufuata elimu

**Na Steven William,** MUHEZA

WANANCHI wa kijiji cha Mikwamba, Muheza mkoani Tanga, wameanza mchakato kuchangishana fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi na darasa la awali, baada ya watoto wao kutembea umbali wa kilometa tatu kufuata elimu.

Hayo yamebainika katika mkutano wa hadhara wa kijiji hicho uliofanyika juzi katika ofisi ya kijiji ukiwa na agenda 13.

Ujenzi huo unafanyika baada ya wananchi kushikwa na uchungu, watoto wao wadogo wa darasa la awali na darasa la kwanza kutembea kilomita tatu kufuata shule ya msingi ya Mbaramo, kitendo ambacho ni hatarishi kwao ama kutumbukia Mto Msangazi au kugongwa na magari.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mikwamba, Rose Mdaki, alisema wakati wowote ujenzi wa shule hiyo utaanza, baada ya kukaa vikao wataanza kuchangishana fedha na kushiriki nguvu kazi ya msalagambo.

# Meneja TANROADS aagwa, kuzikwa Kahama

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

VILIO na simanzi vimetawala wakati wa kuuaga mwili wa Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Mlima Ngaile (55), aliyefariki dunia juzi wakati akishiriki mbio za marathon za Wiloles Foundation 2024.

Mhandisi Ngaile amefariki dunia baada ya kupata mshituko wa moyo wakati akishiriki mbio hizo za kilometa tano kwa ajili ya kuchangisha fedha za kununua vifaa ili kuokoa maisha ya watoto njiti.

Katika ibada ya mazishi iliyofanyika jana katika Kanisa la Katoliki Jimbo Kuu la Songea, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Wilman Kapenjama, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, alisema taarifa za madaktari zinasema alifariki dunia kutokana na mshituko.

Ibada hiyo ilihudhuliwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa chama, serikali pamoja na makandarasi na watumishi wa TANROADS na Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) .

Kapenjama alisema Mhandisi Ngaile amekutwa na umauti wakati akitimiza dhamira yake kubwa ya kuchangia watoto njiti mkoani humo, kwa kushiriki mbio za hisani kama alivyoahidi.

"Kifo kinakatili sana kwa namna kinavyoondoa ndugu zetu. Wako wanaoondoka ghafla kama Mhandisi Ngaile na wako wanaougua na kulazwa hospitalini na kuzidi kupoteza matumaini na baadaye taarifa za kifo zinapotokea tunasema ameteseka sana acha apumzike.

"Hatusemi kifo kama hiki hakiuzunishi, tofauti na hiki kinachotokea ghafla kinaumiza zaidi," alisema.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi kuacha maneno kuwa kuna hujuma imefanyika, hivyo wauchukulie msiba huo ni wa kawaida.

Akiongoza ibada hiyo, Paroko wa Kanisa Kuu Jimbo Kuu la Songea, Padri Daniel Otieno, aliwataka waumini watambue kuwa maisha ni mtihani.

"Tujiandae endapo Felix angejua kuwa katika mazoezi yake ndio ingekuwa mwisho wake, angewaaga marafiki zake kuwa hatorudi, lakini tutambue maisha ni kama maua, asubuhi yana chanua jioni yananyauka," alisema.

Padri Otieno aliwataka pia wananchi mkoani Ruvuma kufanya kazi kwa bidii ikiwa ni pamoja na kujenga tabia ya kumtegemea Mungu kwenye kila kitu wanachofanya.

Akisoma wasifu wa marehemu, Meneja wa TANROADS Songwe, Suleiman Bishanga, ambaye aliwawakilisha mameneja wenzake nchini, alisema Mhandisi Ngaile amefanya kazi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mwanza, Mara na Kilimanjaro.

Alisema hadi anakutwa na umauti alikuwa Meneja wa Mkoa wa Ruvuma na aliripoti kituo hicho cha kazi Oktoba, mwaka jana. Ameacha mjane na watoto watatu.

Mwenyekiti wa Makandarasi Mkoa wa Ruvuma, Charles Mhagama alisema alikuwa na msaada mkubwa kwa wakandarasi na alitatua kero zao kwa wakati mwafaka.

"Kifo ni sawa na mtego. Ni vyema kucheki afya mara kwa mara na tutende mema kama ambavyo marehemu alikuwa akifanya (enzi za uhai wake) ili hata muda wa kuondoka duniani ulifika, tukumbukwe kwa mema kama Mhandisi Ngaile," alisema Mhagama.

Mhandisi Roman Mbukwini, Msimamizi Kitengo cha Matengenezo alisema: "Tumefanya naye kazi vizuri na amekaa miezi minne Songea, wanatarajia kusafiri leo (jana) kwenda wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, kwa maziko yatakayofanyika Jumanne ijayo."

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali Wiloles Foundation, Geofrey Mdede, katika salamu zake za rambirambi, alitoa pole kwa familia na wafanyakazi wote wa TANROADS.

"Tulikuwa naye nusu saa kabla ya kifo chake uwanja wa Majimaji na alishiriki mbio za kilometa tano na baada ya nusu saa mbele, akakutwa na umauti, tumeumia sana na tukio hili," alisema.



Katibu Tawala wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (wa pili kushoto), akizungumza na wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu katika shule ya sekondari ya Kwemkabara, wilayani humo hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Othman ataka viongozi maslahi waepukwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi katika Mkoa wa Kichama wa Kaskazini 'A' Unguja, kuwaepuka viongozi wanaowania nafasi kwa ajili ya maslahi binafsi. Othman ameyasema hayo katika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni , Kaskazini Unguja, alipofungua mkutano mkuu wa uchaguzi wa mkoa huo, ikiwa ni mwendelezo wa uchaguzi katika ngazi hiyo nchini kote.

Alisema uongozi ni dhima na dhamana ambayo viongozi hupewa baada ya kuaminiwa ili kuwatumikia wananchi na si uhasama na biashara na uchumi kama baadhi ya watu wanavyoamini.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema kiongozi anayechaguliwa lazima awe na uchungu na kupenda maslahi ya nchi na wananchi na awe tayari kuwatumikia wananchi kwa uzalendo.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wajumbe wa mkutano huo kutofanya kosa kuchagua viongozi wasiojielewa na wanaotaka kuingia kwenye uongozi kwa manufaa binafsi.

Alisema ni lazima kuwachagua viongozi wanaowaamini na ambao wanafahamu dhamira ya chama na kutetea maslahi ya Zanzibar.

Pia alisema kuna umuhimu kuwaepuka watu wanaoujua ukweli na haki lakini wakakengeuka kwa kufikiri zaidi maslahi binafsi badala ya kuzingatia umma jambo ambalo ni hatari kwa maendeleo ya nchi.

"Wajumbe na wagombea kwa jumla fahamuni kwamba uchaguzi ni utaratibu wa kubadilishana dhamana kama mbio za vijiti na suala hilo kamwe lisiwe sababu ya mifarakano. Baada ya uchaguzi tuendelee kuwa wamoja kwa kufuata falsafa ya chama ya kuchagua mmoja na kubaki wamoja," alisema.

Kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), Othman alisema dhamira ya ACT- Wazalendo ni kuingia kwenye serikali kwa ajili ya kuendeleza amani ya kweli katika kuhakikisha Zanzibar inasonga mbele kimaendeleo kwa maslahi ya wote.

Akizungumzia Muungano, Othman alisema ACT- Wazalendo kamwe haikatai Muungano lakini uwe wenye kuzingatia maslahi yenye uwiano na faida sawa kwa pande zote mbili.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Kwanza wa Rais alisema Zanzibar ina historia kubwa kutokana na neema iliyo nayo toka zamani ndiyo maana mwaka 1971 iliuza karafuu tani 61,000 ambazo ziliingiza Sh. milioni 547 kwa wakati huo.

Pia alisema Zanzibar wakati huo iliuza mapipa ya mafuta ya karafuu na makonyo kwa thamani ya Sh. milioni 16 kwa mwaka huo.

HABARI KITAIFA



Meneja wa Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira vijijini (RUWASA), Mkoa wa Manyara, Mhandisi Walter Kirita akizungumza kwenye mazishi ya dereva wa RUWASA wilaya ya Kiteto, marehemu Sufian Nyanyu, wilayani humo juzi, aliyefariki dunia baada ya gari alilokuwa akiendesha kusombwa na maji mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanaotorosha pamba nje wapewa salamu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WAKULIMA wa pamba Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameonywa kuacha tabia waliyoianzisha msimu uliopita ya kutorosha zao hilo na kwenda kuuza nje ya wilaya.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Given Ngilangwa, alisema jana kuwa, hali hiyo inasababisha Halmashauri kukosa mapato yake kupitia ushuru uliotakiwa kukusanywa kipindi cha masoko kwenda wanapouzia.

Ngilangwa aliyasema hayo wakati akizungumza na wakulima wa zao hilo kutoka Chama cha Msingi (AMCOS) cha Isanja Budugu kilichoko Kata ya Chambo, kama sehemu ya kuwaelimisha namna ya kukabiliana na mvua zisiharibu zao hilo ambalo halihitaji maji mengi.

Aliwataka kuacha kuchanganya pamba na vitu vingine kama mafuta ya kenge, mchanga pamoja na maji kwa lengo la kuongeza uzito na kujipatia fedha pasipo halali.

Alisema kwa kufanya hivyo kunasababisha pia, pamba kukosa ubora unaohitajika na kukimbiwa na wanunuzi na kusababisha kuichafua wilaya katika masoko ya kimataifa.

Alisema msimu uliopita wa 2022/2023 baadhi ya wakulima walitorosha pamba na kwenda kuuza maeneo ya nje ya Kahama zikiwamo Wilaya ya Nzega na Tabora, hali iliyosababisha halmashauri kukosa mapato yake ipasavyo kwani ushuru unaotakiwa kukusanywa wakati wa soko ulibaki katika maeneo hayo.

Aliwakumbusha kuwa mapato yanayopatikana ndiyo yanayosaidia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule za msingi na sekondari, zahanati, vituo vya afya, barabara na huduma nyingine za kijamii. Ofisa Ushirika wa Halmashauri hiyo, Karenga Dismas, alisema mchezo unaofanywa na baadhi ya wakulima wa kuchanganya pamba na vitu visivyohitajika kwa lengo la kuongeza uzito vinasababisha pamba kukosa ubora unaohitaji na kukimbiwa na wanunuzi.

Mjumbe wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Ngamba Bundala, aliyemwakilisha mwenyekiti wake, Tano Nsabi alisema, wakulima waliouza pamba yao KACU wajiandae kupata malipo ya pili muda wowote mwezi huu.

Mkulima wa Isanja Budugu, Zabroni Maduhu, alikiri katika msimu uliopita baadhi ya wakulima walitorosha pamba na kuuza nje ya wilaya.

# Walimu waonywa kutumia vishikwambi kucheza kamali

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WALIMU wilayani Mkalama, Singida, wameonywa kutumia vishikwambi walivyopewa na serikali kwa kucheza michezo ya kubahatisha na kutakiwa kuacha tabia hiyo mara moja.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi, Amina Irumba, alitoa onyo hilo juzi wakati wa mafunzo kwa walimu kuhusu mitaala mipya itakayoanza kutumika kuanzia mwaka huu kwa madarasa ya awali na la tatu.

Irumba alisema walimu watambue kwamba vishikwambi walivyopewa ni kwa ajili ya kujisomea na kujifunza vitu mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wao na sio kuvitumia kwa michezo ya kubahatisha.

Alisema walimu wanatakiwa kuendana na mabadiliko ya teknolojia kwa kutumia mifumo mbalimbali katika kurahisisha utendaji kazi ambapo amesisitiza kuwa makini na taarifa zao za siri.

"Ninawaomba walimu tuwe makini na taarifa zetu maana sasa mnatumia mifumo katika utendaji kazi wenu, wengi wetu bado hatuja 'master' kutumia mifumo hiyo, mnapoenda huko 'stationary' kuweni makini na taarifa zenu za siri hususani kutoa nywira zenu," alisema.

Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule Wilaya ya Mkalama, Ignatus Kinyeje, aliwataka walimu kusikiliza kwa makini na kujifunza namna mtaala mpya utakavyoenda kufanya kazi, ili kuwasaidia kuendana na mabadiliko ya mtaala huo utakaoanza kutumika mwaka huu kwa madarasa ya awali hadi la tatu .

"Leo tunafungua mafunzo haya kwa niaba ya mafunzo yote yanayoendelea leo Wilayani Mkalama, ninawataka walimu kuwa na bidii katika mafunzo hayo, pia mkipata fursa ya kusoma mkasomee masomo ya Kifaransa na Kichina, kwani ndio yameongezwa katika mtaala huu mpya," alisema.

Kinyenje amewataka walimu hao kuwa na bidii katika ufundishaji katika kupandisha kiwango cha ufaulu na kudhibiti suala la utoro kwa wanafunzi, hususani katika kipindi hiki cha muhula mpya wa masomo kwa mwaka 2024.

Maofisa Elimu Wilaya pamoja na Uthibiti Ubora Elimu Wilaya ya Mkalama, wameendelea kukagua hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza kwa kutembelea shule mbalimbali.


ASYLA ATTORNEYS

ADVOCATES, PATENT AND TRADEMARK ATTORNEYS, NOTARIES PUBLIC AND COMMISSIONERS OF OATHS

PUBLIC NOTICE

We are advocates of Paje Beach Resort Limited t/a Serenity Villas **("our Client")**

We refer to the public notice by ACCURATE RECOVERY & AUCTION LIMITED regarding sale of Hotel Beach Villa along Paje Beach property of Paje Beach Resort Limited t/a Serenity Villas. **("the Property")**

**The Public is notified as under, that:-**

1. Our Client has pending court case against Equity Bank Tanzania Limited **("Equity")**, namely Commercial Case No. 3 of 2020; Misc. Commercial Application No. 06 of 2022 and Misc. Commercial Application No. 07 of 2023 all pending in the High Court of Zanzibar Commercial Division Holden at Tunguu -Zanzibar
2. In respect of the Commercial Case No. 3 of 2020 the Honourable High Court issued an ex-parte order barring Equity from disposing the Property pending determination of the dispute between the parties coupled with an undertaking by Equity's advocates of channeling all actions through the Court.
3. In the pending Misc. Commercial Application No. 07 of 2023 our Client seeks similar reliefs of maintenance of status quo pending determination of the dispute between the parties.
4. Our client has learnt with great concern a public notice issued by ACCURATE RECOVERY & AUCTIONS LIMITED in the Guardian Newspaper of 1 January 2024 giving 14 days' notice of sale of the Property and invitation of sealed bids.
5. The public is hereby informed that the Property is subject of court litigation and, as such, the purported loan by Equity and alleged default is a contentious matter. In law and equity, the Property is not ripe for sale.
6. The public is enjoined to desist from taking part in the impugned sale of the Property since it constitutes a wrongful interference with the due process of law and demeans the sanctity of the Court proceedings.
7. Any person who participates in the purported bid does so at own peril for contempt of Court and further legal action against Equity, the auctioneer, and such person who participates in the purported bid process.

For further information kindly contact:

**Managing Partner**
**Asyla Attorneys**
**1st Floor, Alfa House**
**P.O.Box 80496**
**New Bagamoyo Road**
**Dar es Salaam**
**Tel:+255739211176; Email: info@asylattorneys.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upimaji afya uzingatiwe kuepuka vifo vya ghafla

**MAGONJWA** yasiyoambukiza katika miaka ya karibuni, yameelezwa kuwa yanachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya watu na hata kusababisha kupungua kwa nguvu kazi katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo. Miongoni mwa magonjwa yanayotajwa ni shinikizo la juu la damu, kisukari na maradhi ya moyo.

Sababu kubwa zinazotajwa kuwa chanzo cha maradhi hayo ni ulaji wa vyakula bila mpangilio hasa vile vyenye mafuta kwa wingi, mtindo wa maisha, kutokufanya mazoezi na kutozingatia ushauri wa wataalamu wa afya.

Shikinizo la damu na magonjwa ya moyo, kwa mfano, taarifa za kitabibu zinabainisha kuwa yamekuwa yakisababisha vifo vya ghafla watu wakiwa wamekaa, wakifanya kazi au wakiwa wamelala. Pia maradhi hayo yameelezwa kuwa husababisha vifo vya watu hata wakiwa kazika michezo au mazoezi kutokana na kutokupima hali zao kabla ya kuanza shughuli hizo.

Ushuhuda mmojawapo ni wa juzi baada ya Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Mlima Ngaile, kufariki dunia wakati akishiriki mbio za Wiloles Foundation Marathon 2024. Akiwa mmoja wa viongozi waandamizi, alishiriki mbio hizo akijumuika na wenzake kwa ajili ya kuchangia matibabu ya watoto waliozaliwa kabla ya muda (njiti) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma ya Songea (HOMSO).

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Songea, Wiliam Kapenjama, meneja huyo alifariki juzi saa 3:00 asubuhi. Meneja huyo, viongozi na washiriki wengine, walifika katika viwanja vya michezo vya Majimaji na kujisajili kisha wakaanza kukimbia umbali wa kilometa tano. Wakiwa katika mbio hizo, Ngaile aliwapita washiriki wenzake na muda mfupi kidogo alianguka na kupoteza fahamu kabla ya kubainika kuwa amefariki dunia baada ya kufikishwa hospitalini.

Kifo cha meneja huyo wa TANROADS ni kimojawapo ya vile vingi ambavyo vimekuwa vikitokea kutokana na maradhi yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu. Licha ya kwamba ni wachache wanaobainika na kutangazwa, vifo vya namna hiyo ni vingi na kwa kiasi kikubwa vimekuwa vikigharimu maisha ya watu wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa.


Kutokana na ongezeko la vifo vya namna hiyo na vile vitokanavyo na maradhi ya moyo na kisukari, viongozi na wataalamu wa afya, mara kwa mara wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa watu kupima afya zao ili kujua kama wana maradhi hayo ili wapate ushauri na tiba kabla tatizo halijawa kubwa.

Pamoja na ushauri huo, madaktari na madaktari bingwa katika tiba, pia wamekuwa wakiwashauri watu kupima afya zao kabla ya kuanza kufanya mazoezi na kwamba hata kama hawana matatizo kama hayo, wafuate kanuni na taratibu ili kuwaepusha na madhara yanayoweza kujitokeza ghafla na hata kupoteza maisha.

Ni ukweli usiopingika kwamba hivi sasa katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, kumekuwa na mwitikio mkubwa wa watu kufanya mazoezi ya kukimbia au kwenye maeneo maalum, maarufu kama 'Gym'. Licha ya kuwapo kwa mwitikio huo, je, wanafuata ushauri wa madaktari juu ya kupima afya kabla ya kuanza kufanya?

Ni wakati mwafaka sasa kwa Watanzania kuwa mstari wa mbele katika upimaji wa afya ili kujikinga na matatizo yanayoweza kuzuilika ikiwamo vifo vinavyotokana na maradhi ya moyo na shinikizo la damu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Falsafa ya Rais Samia ya R4 yafaa kuigwa

**KATIKA** hatua ya kurejesha hali ya maridhiano, uvumilivu baada ya siasa za uhasama ambazo zilikuwa zimeanza kujitokeza, Rais Samia Suluhu Hassan aliamua kuja na falsafa ya R4.

Rais alikuja na falsafa hiyo ili kujenga nchi ya watu wanaoishi kwa kusameheana, kuvumiliana, kuleta mabadiliko na kujenga nchi kwa pamoja kupitia hiyo falsafa yake ambayo inaendelea kutumika.

Katika falsafa hiyo, ya R4, R ya kwanza ni 'Reconciliation' ikiwa ni maridhiano au upatanisho miongoni mwa wanasiasa na makundi mengine kwa kuwa ni muhimu kwa makundi yote yanayotofautiana.

R ya pili ni 'Resilience' ambayo inahusu ustahimilivu huku R ya tatu ikiwa ni 'Reforms' kwa maana ya mageuzi, wakati R ya nne ni 'Rebuild' ikimaanisha kujenga taifa.

Kimsingi R zote zinagusa umuhimu wa Watanzania kuwa wamoja bila kujali tofauti zao za kisiasa, kuvumiliana, kukosoana na kushirikiana katika ujenzi wa taifa kwa kuzingatia umoja wa kitaifa.

Baada ya kuwapo kwa falsafa hiyo, sasa wadau wa demokrasia wamekuwa wakikutana katika vikao mbalimbali kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya nchi.

Hata wiki hii wadau hao wakiwamo wa vyama vya siasa, walikuwa jijini Dodoma wakitoa maoni yao kuhusu miswada ya sheria ya uchaguzi kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Kuwapo kwa utaratibu huo ambao unagusa pia uhuru wa habari na kujieleza na mikutano kwa vyama vya siasa, ni wazi kwamba falsafa hiyo ya Rais inafanyika kwa vitendo.

Ikumbukwe kuwa tangu aliposhika usukani wa kuongoza nchi mwanzoni mwa mwaka 2021, Rais Rais umebadilisha upepo wa siasa kwa kuruhusu mikutano ambayo awali ilizuiliwa.

Amekutana na makundi mbalimbali kwa lengo la kutimiza falsafa yake ya R4 ambayo imeanza kuzaa matunda kutokana na wigo mpana ambao umekuwapo kwa wadau wa demokrasia kukutana na kujadili mustakabali wa taifa lao kwa uhuru.

Lakini pia kwa ujasiri wake, kwa lengo la kujenga na kuimarisha hali ya demokrasia, Rais aliunda kikosikazi kilichotoa maoni mengi ya namna ya kuboresha demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Miongoni mwa maoni yaliyotolewa ni kufanya marekebisho katika sheria za uchaguzi na zile zinazoratibu shughuli za vyama vya siasa ambazo sasa wadau wanaendelea kuzitolea maoni.

Hatua hiyo ya Rais ilikuwa na utashi wa kisiasa, kwani baada ya kupokea ripoti ya kikosikazi alizielekeza taasisi mbalimbali za serikali kuanza kufanyia kazi mapendekezo hayo ikiwamo kufanya marekebisho ya sheria ambazo sasa zinawatukutanisha wadau wa demokrasia.

Jambo la muhimu ni wadau hao kutoa maoni yao kwa kutanguliza uzalendo mbele kwa kutoa maoni yenye kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa na sio maoni ya kuvunja umoja huo.

Mkutano huo maalumu wa kutoa maoni kuhusu miswada ya sheria za uchaguzi na za vyama vya siasa una umuhimu wake kwani unaakisi falsafa ya Rais ya R4 inayoakisi kuunganisha Watanzania wote.

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu kuhusu mambo mbalimbali katika siasa, kuanzia muundo wa tume ya uchaguzi, wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi, mgombea huru, katiba mpya.

Hivyo, kitendo cha Rais kuunda kikosikazi cha kukusanya maoni kuhusu namna bora ya kufanya maridhiano ya kisiasa ili kujenga taifa lenye umoja na mshikamano ni jambo la msingi.

Ninadhani kwa hayo na mengine mengi, Rais anastahili pongezi kwa uamuzi wake wa kizalendo wa kujenga siasa za nchi kwa kuzingatia mfumo wa sasa wa vyama vingi, kwa njia ya maridhiano na kuvumiliana.

Si vibaya vyama vya siasa vikajenga mfumo wa maridhiano na uvumilivu kupitia falsafa ya Rais ya R4 ili kujenga taifa lisilo na nyufa na matabaka, kwa kuzingatia kuwa wote ni wamoja.

Kwa kuwa Rais ametengeneza mazingira rafiki ya kufanya siasa, viongozi wa vyama vya siasa wanaweza kuiga mfano huo na kuutumia katika vyama vyao ili kuondoa migogoro ndani ya vyama hivyo.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Tuyaenzi Mapinduzi kwa 4R za Rais Samia



Pascal Mayalla

KWANZA nijiunge na Watanzania wenzangu, kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa Zanzibar kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, huku waliopindua wakiyaenzi na kuyaita Mapinduzi Matukufu, na wale waliopinduliwa wakisema hayana utukufu wowote kwa sababu yaliandamana na umwagaji wa damu.

Kutokana na kuwapo kwa kambi hizo mbili, nashauri katika kuyaenzi Mapinduzi haya, tuitumie falsafa ya Rais Samia ya 4R kutibu makovu ya Mapinduzi na kuponya vidonda ambavyo ni vibichi vitokanavyo na Mapinduzi hayo.

Nawaomba Wazanzibari kuielewa na kuizingatia falsafa ya 4R iliyoasisiwa na kutumiwa na Rais Samia katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuyafikia mafanikio na kuwa Zanzibar moja kwa maendeleo endelevu.

Falsafa hiyo ya 4R inahusu mambo manne ya msingi ya kuzingatiwa ambayo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahimilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi mpya (Rebuilding).

Zanzibar ni nchi ya Mapinduzi, hivyo kuna aliyepindua, anayetamalaki kwa shangwe, nderemo, vifijo na shamrashamra zote kusherehekea miaka 60 ya Mapinduzi. Lakini pia yuko aliyepinduliwa na huyu amenyamaza kimya akiumia chini kwa chini na ndani kwa ndani, akikumbuka kilichotokea na yatokanayo na Mapinduzi hayo.

Zanzibar kunahitajika kuundwa Tume ya Mapatano na Maridhiano ili kuwaponya walioumizwa na Mapinduzi yale ili kujenga Zanzibar moja yenye kusameheana, kuleta umoja na amani na maelewano kwa wote. Hali hiyo itahusisha moyo wa kitaifa na kuunganisha nguvu ya pamoja katika kuleta maendeleo endelevu kwa visiwa hivyo vya karafuu.

Natoa wito kwa Rais Samia na Rais Mwinyi, kutumia 4R za Rais Samia kwa kuwasamehe wapinduliwa wote akiwamo Sultan Barghash, kuwajengea mazingira wezeshi wawe huru kurejea Zanzibar ili kushiriki katika ujenzi wa Zanzibar moja yenye uhuru, umoja, upendo, amani, na mshikamano.

Hili likifanyika, Rais Samia na Rais Mwinyi, watabarikiwa sana kwa kuponya machungu ya Mapinduzi Matukufu na Zanzibar itabarikiwa sana.

Japo Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) imeleta mshikamano, bado kuna changamoto mbalimbali zikiwamo za Muungano ambazo zamani zilikuwa zikiitwa Kero za Muungano, kule Pemba wanaziita makero.

Hapa R ya pili ya Ustahimilivu (Resilience) itumike kutatua changamoto hizo za Muungano na kuzigeuza fursa. Wapindua wasinyanyue mabega juu kujiona wao ndio wao na wapinduliwa wasijisikie wanyonge. Wote wawe wastahimilivu katika kuleta maendeleo kwa kuwa katika dunia ya sasa, changamoto haziepukiki kwa sababu ni dunia ya sayansi na teknolojia, huivyo ni lazima tukabiliane na kila changamoto kwa ustahimilivu.

Mfano mzuri wa ustahimilivu ni kwamba japo mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya 2010 yako tofauti na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), madam yote yamefanywa kwa ajili ya Zanzibar, safari hii serikali ya JMT imestahimili. Ilichofanya ni kwa Katiba ya JMT kutofanyiwa mabadiliko kuyatambua mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar, lakini itifaki zote zinayatambua.

Kwa upande wa Mageuzi (Reforms), kiukweli Rais Mwinyi kupitia falsafa yake ya Uchumi wa Buluu, ameibadili Zanzibar kutokuwa watumwa wa historia ya Mapinduzi bali kuirejesha kuwa nchi ya maendeleo makubwa eneo hili la Afrika Mashariki. Zanzibar ilikuwa nchi ya kwanza barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na televisheni ya rangi mwaka 1971, Rais Mwinyi anafanya mageuzi mengi yanayoipaisha kitaifa na kimataifa.

Nikimalizia na dhana ya Ujenzi Mpya (Rebuilding), Rais Mwinyi anafanya mengi makubwa kwenye kuijenga upya Zanzibar lakini umuhimu ni kujifanyia tathimini kwa kuangalia kasoro au upungufu uliopo na kuzifanyia kazi hatimaye kusonga mbele katika kusukuma maendeleo

Rais Samia ilichokifanya kwa Tanzania hususan Tanzania Bara, Rais Mwinyi akifanye Zanzibar katika hali ya maelewano, usalama na maendeleo endelevu kutokana na siasa za uhasama zilizorithiwa kwa sababu ya historia ya vyama vingi na kasoro mbalimbali ndani ya vyama vya upinzani pamoja na serikali.

Aidha, Rais Samia ameamua kujenga nchi yenye Watanzania wanaoishi kwa kusameheana, kuvumiliana, kuleta mabadiliko na kujenga nchi kwa pamoja. Mpango mkakati huu wa R4 za Rais Samia umesaidia sana kuleta taswira mpya na nzuri kwa Tanzania kitaifa na kimataifa. Kwa hilo nasema kongole Rais Samia.

Uongozi imara wa Rais Samia umefanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa vyama vya upinzani, makundi mbalimbali, asasi za kiraia na matunda ya upatanishi yanaonekana katika jamii ya Watanznaia. Viongozi wakuu wote wa vyama vya upinzani wameonyesha kufurahia na kuunga mkono juhudi hizi za Rais Samia kwenye sera zake pamoja na nia yake ya kuikwamua Tanzania iliyokuwa imekwama na sasa tunakwenda kuwa na sheria mpya ya uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi na uwanja sawa wa kufanya siasa.

Kinachofanyika Tanzania pia kifanyike Zanzibar. Rais Mwinyi akae na wapinzani wafanye mapitio ya maridhiano ili uchaguzi wa Zanzibar wa 2025 uwe huru na wa haki na mshindi halali atangazwe.

Mwisho ni ombi kwa Rais Samia. Ili hizi 4R zilete manufaa ya kweli, lazima tufanye mabadiliko madogo ya Katiba ya JMT, tuwatendee haki Zanzibar kwa madadiliko ya katiba yao ya 2010 yatambuliwe na katiba ya Tanzania.

**Paskali +255 754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Watanzania tumakinike na 'madaktari' na 'wauguzi' hawa



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HUU ni mwaka wa siasa zaidi, tena unaojiandaa kuukabidhi mwaka ujao mzigo mzito zaidi wa kisiasa kwani yote ni ya uchaguzi utakaowapa Watanzania viongozi wanaowataka, endapo mambo yatakuwa kama ilivyopangwa na wengi.

Nchi yetu imejigawa katika makundi matatu makuu kama ilivyo katika tasnia ya afya na tiba; kuna madaktari, wauguzi na wagonjwa. Madaktari ni wale walioko juu wanaoendesha hospitali (nchi) wakisaidiwa na wauguzi wao.

Huku nje ndiko tuliko sisi wananchi ambao ndio wagonjwa, tukitegemea hospitali kurekebisha hali za afya zetu kwa kupata tiba lakini sauti ya juu ikisubiriwa kutoka kwa daktari ambaye ndiye anashikilia uhai wetu.

Tanzania kwa sasa madaktari ni viongozi wa serikali wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakisaidiana na wauguzi ambao ni wapinzani wanaosubiri kusikia daktari anasema au anaagiza nini.

Kuna nyakati daktari atatoa maagizo ambayo muuguzi anaona hayastahili kwa mgonjwa, lakini kwa kuwa hakushika mpini, inabidi atekeleze kwani asipofanya hivyo, mgonjwa akipoteza maisha, lawama zitamwangukia yeye.

Ndiyo sababu, unaweza kusikia kwenye korido za hospitali, wauguzi wakiwasema madaktari wao, kuwa hawafanyi inavyostahili na hivyo kuacha mambo yaende kama yalivyo, kwa kuzingatia mwongozo wa ajira na maadili ya hospitali.

Kuna nyakati muuguzi anaona kabisa daktari kakosea lakini akitaka kuchukua hatua ya kurekebisha ni mara chache mgonjwa kumkubalia amfanyie upasuaji kwani si daktari hata kama ana uzoefu.

Si ajabu muuguzi kumfanyia upasuaji mgonjwa hata kama si daktari kwani kutokana na uzoefu anaweza kufanya na mgonjwa akapona, ingawa atakuwa amekiuka maadili na taratibu za kazi.

Kuna simulizi ya walinzi wa uwanja wa ndege mahali fulani Afrika ambao usiku walikuwa wakizirusha kwenda viwanja jirani wakiuwa na abiria na kujipatia kipato haramu, mpaka siku mmoja alipoangusha moja.

Yote hayo yalifanyika kwa utundu wa kuzoeana na marubani na kujifunza kidogo kidogo huku siku zingine wakiachiwa kuziegesha. Yanaweza kufanywa na wauguzi hospitalini, kwa kujivika udaktari na kutibu. Mbona kuna hata mawakili bandia wanaoshinda kesi kibao!yo yana

Sasa tumeingia kwenye mwaka ya uchaguzi, mwaka huu tukianza na serikali za mitaa na mwakani tukichagua rais, wabunge na madiwani. Ni mtihani mgumu sana kwetu wagonjwa, tunapoangalia madaktari waliopo lakini pia wauguzi tulionao.

Yawezekana kabisa kwenye uchguzi wa mwaka huu, mambo yakiwa mazuri na mazingira rafiki ya uchaguzi, inawezekana uchaguzi usiwe mgumu sana, hasa wananchi wakiachwa waamue wanachokitaka kuliko kujsimamiwa mgongoni na hata kushikiwa akili.

Lakini mwakani kuna mtihani mgumu hasa kwa kuangalia nani na nani watatakiwa kuwa wabunge na madiwani, lakini pia rais wa nchi, ingawa kule kwa madaktari, tunaambiwa daktari mkuu ataendelea kuwa Dk Samia Suluhu Hassan mpaka 2030.

Hata hivyo, chini kwa chini tunaambiwa kuna watu wanautamani udaktari mkuu na wakipata upenyo wanaweza kuusaka huku na sisi wagonjwa, tukiangalia pia miongoni mwa wauguzi nani anastahili nafasi hiyo.

Ukweli usio na mawaa ni kuwa tukimweka pembeni Dk. Samia, halafu tukasema sasa apatikane daktari mwingine wa kuongoza hospitali hii, ni mtihani mpevu? Dk. Mwigulu Nchemba? Dk. Januari Makamba? Dk. Nape Nnauye? Dk. Emmanuel Nchimbi? Angalau baadhi walishajitosa huko nyuma. Wanaweza kuwapo wengine.

Huku kwa wauguzi tuna Dk. Freeman Mbowe, Dk. Zitto Kabwe, Dk. Ibrahim Lipumba, Dk. James Mbatia, Dk. Tundu Lissu, Dk. Hashimu Rungwe; hawa ndio wanaotajwatajwa. Nani sasa hapa anastahili kuwa Daktari Mkuu? Nia hapa yawezekana kuwapo wengine.

Sasa tujiulize Watanzania, katika hawa kuna mmoja tunayedhani anaweza kuongoza hospitali yetu hii na tukapata matibabu mazuri na kuondokana na maradhi yanayotusumbua kwa miaka yote hii?

Ni wazi kuna wasiwasi na shaka dhidi ya wauguzi kutoka kwa wagonjwa, kuwa pengine hawawezi kuisimamia hospitali hii, kutokana na wanavyoonekana kushindwa kuwasemea na kuwasimamia vizuri katika mambo yao.

Wote madaktari na wauguzi, wengi wao wanaonekana kuwania kuongoza hospitali hii, ili kukwapua dawa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati zao kwingine na kuacha hospitali bila dawa wala vifaa na wagonjwa sisi kuendelea kugugumia.

Kwa hiyo, Watanzania tuna jukumu kubwa sana la kukaa na kubungua bongo na kuwatazama viongozi wetu wa kisiasa kwa umakini mkubwa, ili tusijefanya makosa katika uchaguzi ujao, na ni vema ikatoka ruhusa ya wagombea binafsi.

Bila ruhusa hiyo, tukiendelea kujibana kwenye tandabui za kisiasa kuwa bila kuwa na chama hujagombea, huku asiye na chama akichagua, tutajikuta na mzigo wa madaktari na wauguzi hao na kukosa uwanda mpana wa kupata viongozi. Wagombea binafsi muhimu kipindi hiki ambacho vyama 'havina' watu!

MAKALA

# Falsafa ya 4R ya Samia inawaunganisha Watanzania

Na Kambi Mbwana



Rais Samia Suluhu Hassan

JANUARI 3, mwaka huu, wadau na wanasiasa wa vyama vya siasa nchini walifanya Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama Vya Siasa kujadili Miswada ya Sheria za Uchaguzi na Vyama vya Siasa, uliofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) , Dar es Salaam.

Mkutano huo ulifanyika ukiwa na shabaha mahususi ya kuboresha mazingira ya ufanyaji wa siasa wakati huu ambao nchi inajiandaa kuingia kwenye chaguzi za serikali za mitaa na vijiji mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwakani.

Hoja mbalimbali zilijadiliwa na wanasiasa walioalikwa kushiriki kwenye mkutano huo uliohudhuriwa pia na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othaman Masoud Othaman, Waziri wa Nchi , Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama. Viongozi kutoka vyama vyenye usajili wa kudumu nao walipata nafasi ya kuhudhuria mkutano huo ambao si tu ulikuwa na lengo la kuboresha mazingira ya kisiasa, bali shauku ya kuwaunganisha Watanzania bila kujali itikadi zao.

Kufanyika kwa mkutano huo ni matokeo mazuri kutokana na Watanzania wanavyounganishwa na falsafa ya 4R ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Falsafa hii yenye tija kwa taifa, inakwenda na maneno manne mazito ambayo kwayo yamekuwa dira na mwelekeo sahihi wa siasa za nchi yetu.

Akiwa na shauku ya kuponya majeraha yaliyochangiwa na kuibuka kwa siasa za chuki na uhasama, Rais Samia aliibuka na msimamo wa R4 kwa maana ya Reforms (mageuzi), Reconciliation (Maridhiano), Reform (Mageuzi), Resilience (Ustahimilivu) na Rebuilding (kujenga upya).

Kabla ya kuamua kuirudisha nchi katika mwelekeo huu, Watanzania wanakumbuka lilivyogawanyika vipande vipande. Wakati wote wa utawala wa Awamu ya Tano chini ya Hayati Dk. John Magufuli, hakuna mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) aliyeiva chungu kimoja na wenzao kutoka upinzani kama vile Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama Cha Wananchi (CUF), NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo.

Ni wakati huu ambao jamii ilishuhudia viongozi na makada wa vyama vya upinzani wakishinda au kulala kabisa kortini kwa sababu tu wamejaribu kutoa maoni yao ya namna gani ya nchi inapaswa kuendesha siasa zake. Wachache walionusurika kuburuzwa kortini walilazimika kukimbilia uhamishoni.

Mwanasheria machachari na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, alitimkia Ubelgiji Novemba 10, 2020 huku Godbless Lema aliyewahi kuwa Mbunge wa Arusha Mjini kupitia CHADEMA naye akijisalimisha Canada Novemba, 2020, akipitia Kenya alikokaa kwa takribani wiki mbili kabla ya kupata upenyo wa kuhamia huko.

Haya na mengine mengi ndiyo sababu iliyofanya nchi igawanyike kwa misingi ya kisiasa. Wana CCM waliona wapinzani wanakengeuka, hivyo walistahili kibano kutoka kwa watawala na waliokuwa upinzani wakidhani CCM inatawala nchi kimabavu.

### MWANZO WA ENZI

Hayo yalikoma baada ya Rais Samia kuingia madarakani Machi 17, 2021 siku mbili baada ya kifo cha Dk. Magufuli. Pamoja na mambo mengine, Dk. Samia aliamua kuiponya nchi na kuwaunganisha Watanzania ili wafanye kazi kwa ushirikiano kwa maslahi ya taifa.

Hili limeituliza nchi. Ingawa bado kuna changamoto, angalau kama taifa lina kitu cha kujivunia kutoka kwa Rais Samia. Kama hiyo haitoshi, haoni sababu ya kudhibiti midomo ya wapinzani wake.

Zaidi ya hayo, hoja inayofikia kuigawa nchi, huwa wa kwanza kuiwasilisha mezani kwa ajili ya uchambuzi wa kina. Kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na sheria mbalimbali zilizowekwa, Rais ana mamlaka ya kuamua.

Hata kuamua kupeleka mezani ili lijadiliwe na kufikiwa uamuzi wa pamoja na busara za hali ya juu. Baadhi ya hoja ambazo Rais Dk. Samia aliamua kuwapa watu nafasi ya kuzijadili ni pamoja na kamati ya kuratibu janga la UVIKO- 19. Kamati hii iliyoundwa na Rais Aprili 6, 2021 na kuongozwa na Mwenyekiti wake, Profesa Said Aboud kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Kamati nyingine iliyoundwa na Rais Samia ni ile ya kutathmini utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuiwezesha kutekeleza malengo ya Serikali katika kukuza diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa kimataifa. Kamati hii iliongozwa na Balozi Yahya Simba, aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Zambia.

Awali, kamati hii ilitangazwa Machi 29, 2023 na kuzinduliwa rasmi Machi 31, 2023 huku wajumbe wake wakiwa Balozi Ramadhan Mwombe, Balozi Dk. Mwanaidi Maajar, Balozi Peter Kallaghe na Balozi Tovako Manongi.

Kamati ni nyingi na zote zilionyesha matunda na ustawi mzuri kwa taifa. Kwa kurejea kwenye msingi wa hoja ya 4R ya Rais Samia, hasa katika msingi mama wa siasa na demokrasia ya nchi hii, bado inaonekana picha nzuri kutoka kwenye utendaji wake.

Akiwa na shauku ya kuona nchi hii inatawalika, Rais Samia alimwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa kukaa mezani na wadau wa vyama vya siasa ili kuona namna gani nchi itaendesha siasa za kistaarabu kwa maslahi mapana ya Watanzania wote.

Matokeo ya ushauri wa Rais kwa Ofisi ya Msajili ni kikao cha pamoja cha wadau kilichofanyika Septemba 11, 2023 na kuhudhuriwa pia na Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa na wadau wa demokrasia, Juma Ali Khatibu. Bila kuficha, alionyesha hisia nzuri kwa Rais Samia kwa jinsi alivyoonyesha shauku ya kuipeleka mbele nchi kutoka kwenye mkwamo wa kidemokrasia.

"Baraza la Vyama vya siasa linakupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuimarisha demokrasia na kutunza amani ya nchi. Tunakushukuru kwa kufungua na kutoa ruhusa ya kufanyika mikutano ya hadhara. Kabla ya yeye kuwa Rais, vyama vya siasa nchini havikuwa na fursa hiyo kwa miaka sita iliyopita," alisema Khatibu wakati anawasilisha mbele ya wajumbe wa mkutano huo maalum, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

### AMWAGIWA SIFA

Haya ni miongoni mwa mambo mazuri yanayofanywa na Rais Samia, hali inayosisimua watu ndani na nje ya nchi. Mwanasiasa maarufu nchini Kenya, George Luchiri Wajackoyah, anamwelezea Samia kuwa ni mmoja wa viongozi mahiri waliowahi kutokea Afrika.

Mtazamo wake ulikuja baada ya kuonyesha matumaini makubwa kiasi cha kurudisha hata watu waliokuwa tofauti na serikali ya chama chake, wakati akiwa Makamu wa Rais. Muundo na sera nzuri ziliponya majeraha na kuwafanya Watanzania wote wawe kitu kimoja.

"Rais Samia ni kiongozi wa kuigwa Afrika kwa sasa. Amekuwa mtetezi wa uhuru wa kujieleza na demokrasia. Nampongeza Rais Samia, mimi namwita Simba wa demokrasia na napenda Kenya tumuige maana anafanya kazi nzuri," alisema Wajackoyah mwanasiasa maarufu wa Kenya ambaye anajinasibisha kama mmoja wa watu waliofanikisha wazo la Lema kutorokea Canada wakati wa utawala wa Magufuli.

Ndiyo maana nasema falsafa ya 4R ya Rais Samia inawaunganisha Watanzania wote na kuwa kitu kimoja. Hali hii haikuwepo katika kipindi cha utawala wa mtangulizi wake. Kama taifa, Watanzania wanapaswa kujivunia na kutembea kifua mbele na kumsemea mazuri kadiri watakavyoweza.

**kambimbwana7@gmail.com 0712053949**

# MAISHA

JANUARI 14, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




**Juisi ya lozera na nanasi**

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Ng'arisha kitanda chako namna hii




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# NGOZI BILA MICHIRIZI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | N | D | I | Z | I |
| H | ■ | ■ | ■ | G | ■ | G |
| I | ■ | T | I | I | ■ | I |
| M | T | I | ■ | Z | N | Z |
| O | ■ | N | A | O | ■ | A |
| N | ■ | G | ■ | ■ | ■ | N |
| I | B | A | N | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DAI, MBU, EDA, KAA, CHUKI, DAMKA, OTANA, USIKU, MAPENDO, ICHACHE

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama konokono wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora ununulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**

Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kwa nini mkopo uhonge wanaume?

KARIBU msomaji tuendelee na mada zetu. Kuna swali nimeulizwa na mmoja wa wasomaji wetu kwamba kwa nini baadhi ya wanawake huhonga wanaume fedha za mkopo, matokeo yake wanashindwa kurejesha inavyotakiwa?

Mfano, mwanamke mmoja alichukua mikopo sehemu kadhaa, kisha akaingia mtini, jambo ambalo lilishangaza wengi. Swali likaja kwamba huu ni ujasiriamali au utapeli?

Nimebahatika kuzungumza na baadhi ya watu kupata maoni mbalimbali huku wakikemea tabia ya wanaochukua mikopo na kukwepa kuirejesha. Hebu sikia michango yao hapa chini.

Mmoja akasema: "Huo ni utapeli mkubwa. Alichofanya huyo mama hafai kuigwa katika jamii yetu ya Kitanzania. Utapeli huo utampeleka katika maangamizi ya maisha. Asante kwa mada nzuri."(Shija S.D.L, Tumaini Iringa).

Naitwa Lolita Charles wa Arusha: "Watu kama hawa hawafai katika jamii kwa sababu wanaweza kusababisha wanawake wote tusiaminike. Ushauri wangu ni kwamba bora uishi masikini lakini sio kufanya hivyo."

Andrea Sebastian wa Dar: "Watu kama hao wanatumia jina la ujasiriamali kama kigezo cha kujipatia umaarufu hivyo hawafai katika jamii."

"Nilimdhamini dada mmoja nikamwandikia andiko la mradi (project proposal) akapewa Sh. milioni tano na kaka yake. Alipozipata tu 'akamuoa' mume wa mtu na hela ilipoisha mwanamume akarudi kwa mkewe na yeye akabaki na fremu tupu dukani kwake akidai karogwa na ndugu zake wakamtenga.

Ingekuwa mkopo wa benki ningekuwa jela kwa kumdhamini ila kaka mtu alikuwa anajitoa lawama kwamba hasaidii ndugu ndio maana siku ya kumkabidhi fedha aliwaita ndugu zake wote. (Usitaje jina langu wala simu. Maisha ndivyo yalivyo)".

Mpenzi msomaji hayo ndiyo yalikuwa maoni yao. Lakini msomaji wa mwisho ningependa nimjadili zaidi kwa ujumbe kuhusu wale wanaochukua mikopo kisha kutafuta mahusiano ya muda, na kutafuna mikopo hiyo halafu wanaishia kusaga meno.

Tumulike, dada aliyedhaminiwa mkopo wa Sh. milioni tano alizompa kaka yake, badala ya kwenda kujaza vitu dukani kwake akatafuta mume wa mtu na kwenda kujirusha naye. Zilipoisha mume yule akamrejea mkewe na kumuacha bibie akilalama karogwa. Hivi huyu karogwa au amejiroga mwenyewe?

Ebo! Wakati wakijirusha kijiwe kimoja hadi kingine huku agizo la lete moja moto na moja baridi, lete kuku chipsi, nyama choma na ndizi mzuzu je, hakujua fedha zinateketea na wala hazizalishi? Huu ndio ujinga walio nao kinamama wengi wasiofikiri mara mbili mbili kabla ya kuchukua maamuzi. Mikopo ni mtego na inahitaji nidhamu ya hali ya juu.

Tabia ya wanawake kuhonga wanaume imekithiri sana. Wakati mwingine ni vigumu sana kujua maudhui yake kwani inachangiwa na mambo mchanganyiko. Katika hali ya kawaida kabisa, sijui niseme ni utamaduni uliozoeleka, wanaume ndio tunaojua huwahonga vitu mbalimbali wanawake.

Lakini mwanamke anapomhonga kitu mwanaume, lazima iwekwe alama ya ulizo(?). Na ikifikia hapo, ujue lipo jambo linalolazimishwa hapo. Labda mwanamke anayehonga au kumrubuni kitu mwanaume anataka hisani ya kitu fulani, yawezekana ni mahusiano wakati mwingine ni kampani tu ya kuwa pamoja kwa nyakati fulani.

Msomaji, kwa mfano wapo baadhi ya wanawake ambao hujipendekeza kwa wanaume ili wapendwe. Na hii inatokana na yeye (mwanamke) kumzimia mwanaume fulani.

Angalia huyo bibie tuliyemzungumzia hapo juu. Kadhaminiwa mkopo ulioaminika atautumia kununulia bidhaa za dukani kwake, lakini alivyopata zile milioni tano akamtafuta mchuchu, tena mume wa mwanamke mwenzie. Wakaenda kuzitafuna na zilipoisha bwana akarudi kwa mkewe na bibie akabaki analalama ati karogwa. Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mwingine anaye mume na wanawe, lakini bado anamzimia mume wa mwanamke mwenzie. Kisa anazo fedha zinazomzuzua hivyo kuzitafutia matumizi ya pembezoni na kuwahonga wachuchu awapendao. Ati anaponda raha kwa kubadilisha 'milo'. Huyu kama siyo anaisaliti familia ni kitu gani?

Lengo la mikopo ni ili kuinua mhitaji kiuchumi na siyo kwenda kufanya starehe. Wengine wamejikuta matatani kwa kuchukua mikopo iwe ni kupitia mabenki au vikundi vya kukopeshana na kwenda kulipia mahari, kujengea nyumba bila kuwa na mfumo mzuri wa kurejesha.

Kama huna nidhamu ya kuchukua mkopo na kurejesha ni afadhali usiingie kwenye utaratibu huo.

**Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Viuatilifu vina mchango ndoa nyingi kuvunjika

DAWA za kuua wadudu au viuatilifu ni vitu au kemikali zinazotumika kufukuza, kuharibu na kudhibiti wadudu, magugu au viumbe vingine vinavyoathiri ukuaji wa mimea.

Ingawa ni bora, dawa za kuulia wadudu zina kemikali zenye sumu ambazo zinaweza kuwa na athari kubwa na wakati mwingine sugu kwa viungo vya hisia vya binadamu na mfumo wa neva.

Matumizi holela ya viuatilifu katika mazao, mboga na matunda yanasababisha ugumba kwa wanaume na tezi dume wakati kwa wanawake yanasababisha magonjwa ikiwamo saratani ya matiti.

Asilimia 47 ya mboga zote zilizochukuliwa sampuli katika masoko mbalimbali, zilikutwa na masalia mengi ya viuatilifu na kuashiria kuwa kulikuwa na matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu.

Fanya uchunguzi mdogo tu utabaini kwamba mchicha, sukuma wiki, kabichi, karoti na spinachi nyingi zinazalishwa kwa kutumia viuatilifu ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu.

Matumizi ya viuatilifu yasipodhibitiwa vizuri yanaweza kuingia katika damu kupitia chakula na kuleta madhara makubwa.

Aidha, iwe kwa sumu hiyo kuharibu mfumo wa homoni na kuathiri mfumo wa uzazi wa wanaume, kwa kukata mikia ya mbegu za kiume na kusababisha ashindwe kutungisha mimba.

Kuna madai kwamba zimekuwa zikisababisha ndoa nyingi kuvunjika kutokana na kushindwa kupatikana kwa zao la ndoa, ambalo ni watoto.

Kwamba wanawake wakiathirika zaidi kwa kutuhumiwa kuwa ndiyo chanzo cha tatizo, ambalo si wao waliosababisha, bali lipo kwa mwanamume.

Wakati hayo yakielezwa, tunaambiwa wako wafanyabiashara wenye maduka ya viuatilifu wanauza sumu hizo kwenye maduka ama yliyoko kwenye msongamano wa watu, au masoko ya walaji na katikati ya miji.

Jambo hili halikubaliki kisheria. Swali la kujiuliza, ni kwa nini wakaguzi Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), hatuwasikii mara kwa mara wakipambana na wafanyabiashara hawa ili kuzuia matumizi ya viuatilifu tishio?

Nimeguswa kuandika haya baada ya kumsikiliza Ofisa Sheria Mwandamizi wa TPHPA, Elizabeth Swai, akiwaeleza wakaguzi kuwa wanapaswa kushughulikia tatizo hilo kwa kuwa wana meno ya kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Sheria inaelekeza kwamba mtu atakayekutwa amevunja Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu, adhabu zimetajwa katika kifungu cha 59 cha Sheria ya Afya ya Mimea, Namba 4 ya Mwaka 2020.

Adhabu kwa mtu binafsi faini ya kuanzia Sh. 50,000 mpaka Sh. milioni 10 au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu jela.

Na kwa kampuni, adhabu yake ni kuanzia Sh. milioni 10 mpaka milioni 500; au miaka mitatu jela, endapo atashindwa kulipa hiyo faini.

Licha ya adhabu hizo, TPHPA inaweza ikamfungia kabisa mfanyabiashara aliyekutwa na kosa hilo.


Endapo mtu atakutwa na viuatilifu ambavyo havikidhi matakwa, TPHPA inaweza kutoa notisi kwamba anapaswa ateketeze kwa gharama zake mwenyewe, baada ya kupata maelekezo kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Kifungu cha 50 cha Sheria ya Afya ya Mimea, Namba 4 ya Mwaka 2020, kinaelekeza kuwa mtu yeyote anayesafirisha viuatilifu, hapaswi kuvichanganya na vitu vingine, ama vyakula, nguo au vitu vingine vinavyoendana na hivyo.

Vilevile, kifungu cha 51 cha sheria hiyo, kinaelekeza kwamba maduka ya viuatilifu au sehemu yeyote ya kuhifadhia viuatilifu, hayapaswi kuwa karibu na shule, hospitali, vyanzo vya maji au maeneo ya kuuza vyakula na sokoni.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com. Simu ya mkononi: +255 715 545 490**

# HARUSI











Mwaka 2024 umeanza kwa kasi na hata katika suala la kupendeza katika harusi ni jambo la kuzingatia sana. Pichani ni baadhi ya magauni ambayo yanatamba katika harusi mbalimbali

## MITINDO







# KOTI LA MVUA

## Jikinge mwili na mvua za El nino

MVUA za El Nino zinazidi kunyesha nchini kote, watu wanashauriwa kujikinga kama tahadhari ili kuepuka kupata magonjwa mbalimbali yakiwamo ya mfumo wa upumuaji.

Koti la mvua ni vazi linalofaa katika kipindi hiki kwa ajili ya kuzuia mwili na nguo kuloana maji.

Makoti ya aina hii yamekuwa yakitengenezwa kwa kitambaa chenye ubora wa hali ya juu kinachozuia maji kupita.

Pia koti linaambatana na kofia yenye uwezo wa kurekebishwa kwa kutumia kamba kwa ajili ya kuzuia upepo na mvua isiingie.

Mifuko miwili ya mikono yenye zipu na mfuko mmoja wa kifuani hutoa nafasi kuhifadhi vitu kama funguo, sarafu na simu.

Kitambaa cha Polyster cha asilimia 100 hutumika kutengeneza koti la aina hii, huku chini ya bega huwekwa ili kuwa laini wakati mtu anapovaa.


Koti la mvua la wanaume limeshonwa kwa umakini ili kutoa ulinzi na faraja katika hali ya hewa ya mvua.


Mbele eneo la katikati kuna zipu isiyopitisha maji, iliyowekwa kifuniko cha ndani ambacho huzuia unyevu kupita.

UREMBO

Na Mary Geofrey







# NGOZI BILA MICHIRIZI

TATIZO la michirizi kwenye ngozi linawatesa wanawake wengi hasa katika maeneo ya mikononi, mapajani na tumboni.

Baadhi yao huipata baada ya kubeba mimba hutokana na kuongezeka uzito wa mwili.

Kuna njia mbalimbali za kuondoa michirizi mwilini, ikiwamo kutumia dawa za viwandani na za asili.

Miongoni mwa njia za asili ni pamoja na kula lishe bora muda wote.

Wataalamu wanasema kuna uhusiano kati ya uzito mkubwa na kitambi kupata tatizo la michirizi.

Hivyo punguza vyakula vya wanga na sukari na unashauriwa kula zaidi vyakula kama nyama, parachichi, nazi, samaki na mafuta ya nazi.

Weka ratiba ya kupunguza unene uliopitiliza kwa kufanya mazoezi na kuushughulisha mwili wako.

Tumia protini aina ya collagen, ambayo inapatikana kwa wingi kwenye supu ya mifupa. Supu ya mifupa ina amino acid kwa wingi ambazo hutengeneza collagen inayosaidia kuimarisha tishu za ngozi na kuondoa tatizo la michirizi.

Kitu kingine kinachoweza kukusaidia kuondoa michirizi ni kujipaka mafuta ya nazi mwilini.

Tumia mafuta haya kupaka mwilini unapotoka kuoga na kuepuka kutumia krimu za madukani ambazo ni ghali na baadhi zina madhara.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya lozera na nanasi

JUISI ya lozera ina wingi wa madini chuma yanayochangia uzalishaji wa damu mwilini.

**Mahitaji**

Nanasi moja, lozera kiasi, tangawizi na sukari

**Namna ya kutengeneza**

Menya nanasi vizuri na chukua maganda yake weka kwenye sufuria safi, weka na majani ya lozera na sagia tangawizi kiasi, kisha weka maji na bandika jikoni kuanza kuchemsha hadi yatokote kabisa.

Epua na yachuje kundoa maganda ya nanasi, tangawizi na lozera na kisha chukua brenda na anza kusaga vipande vya nanasi ulivyokuwa umemenya.

Baada ya kusaga chuja juisi na imimine kwenye juisi ya lozera uliyoichuja na changanya vizuri juisi yako.

Onja kama sukari ya nanasi imekolea na kama unaona haitoshi ongezea kiasi unachopendelea na mimina kwenye glasi na uongeze barafu tayari kwa kunywa juisi yako kwa kushushia na chakula chochote unachopendelea.





MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Ng'arisha kitanda chako namna hii

USAFI wa kitanda ni jambo muhimu ambalo linapaswa kufanywa kila siku katika nyumba.

Pia kufanywa muda wowote ndani ya siku hiyo moja kwa kutegemea matumizi yake ilimradi kionekane kisafi wakati wote kwa sababu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba.

Msingi mkubwa wa usafi wa kitanda hiki ni lazima uanzie nyakati za asubuhi unapoamka.

Usafi ninaouzungumzia hapa ni kuanzia kutandika mashuka, kukifuta vumbi katika pande zote zinazokizunguka na kukipangilia vizuri.

Shughuli hizo zote ili zifanikiwe kwa umakini na ustadi zaidi, zinapaswa kufanyika muda mfupi baada ya kuamka na si vinginevyo.

Uzoefu unaonyesha kwamba mtu anapoamka na kuanza kutandika kitanda bila kuchelewa ama kufanya shughuli za nyumbani anaweza kufanya vizuri zaidi kuliko akisubiri kwanza afanye usafi wa kinywa.

Hata kama atafanya baadaye, anaweza asifanye kwa umakini au ustadi zaidi kama inavyokuwa anapoamua kufanya hivyo muda mfupi baada ya kuamka.



Kwa sababu kitanda ni moja ya vitu vinavyoifurahisha nafsi katika nyumba na kiafya, pia ni vizuri kikapewa kipaumbele kikubwa.

Na ili nafsi yako ifurahi kweli na kukusaidia upendelee kuwapo nyumbani mwako kuburudisha macho, kuna umuhimu wa kuhakikisha unakitendea haki kitanda kwa kukifanyia usafi na kukitandika vizuri.

Kinachohitajika zaidi hapa ni ubunifu au umaridadi na kuweka ubunifu zaidi. Kwa mfano kama uwezo wako unaruhusu, si vibaya pia kama mashuka yako unayotandika kwenye kitanda yakaendana na mapazia yako. Hii ni kwa ajili tu ya kuking'arisha zaidi chumba chako. Kwa maana hiyo, kama umetandika shuka la pinki, basi ni vyema mapazia yako yakashabihiana.

Inawezekana ukatenganisha shuka lako unalotumia kulalia na ambalo unalitumia katika shughuli hiyo ya kutandika , hapo uwezo wako kiuchumi ndio utaamua.

Pia kuna mbinu nyingi za kukifanya kitanda chako kiwe katika hali ya usafi na mvuto wa kipekee na uepuke kukiacha kichafu hata kama si kwa kufuata hayo niliyasema.

Kumbuka kila kitu kinahitaji ubunifu. Jitahidi kuongeza ubunifu kila siku kutafuta namna bora ya kukifanya kitanda chako kipendeze kwa sababu lengo kubwa ni kukipendezesha chumba kwenye nyumba yako, nafsi na ustawi wa afya yako pia.

## DONDOO

### Badili mwonekano wa ukuta kwa 'wall paper'

**Na Restuta James**

'WALL PAPER' ni pambo linaloweza kubadili mazingira ya nyumba kwa kiwango kikubwa mno kutokana na aina ya picha zinazotengenezwa kupata aina hiyo ya pambo.

Mwaka 2024 umeanza kwa aina mpya ya wall paper ikiwamo picha inayoonesha jua likizama, ambayo ukiiweka ndani unapata mandhari nzuri.

Iko picha nyingine ya fukwe ikionesha kujaa kwa maji ambayo inaleta mazingira ya utulivu wa hali ya juu.

Mandhari nyingine inayobamba kwenye aina hii ya pambo ni picha ya msitu au bustani ya maua mazuri. Pia picha inayoonesha barabara au mbuga ya wanyama.

Mtaalamu wa mapambo ya nyumbani, Brigitte Didas, anasema picha inayoonesha jua likizama inafaa ile ambayo imepigwa kwa kuchukua mazingira ya mto au maji na aina kiasi ya miti.

Anasema nyingine ni inayoonesha zaidi mawingu na hasa iliyopigwa kwa juu na mtu akiwa ndani ya ndege.


Kwa mujibu wa Brigitte, picha ya msitu inawafaa watu wanaopenda mazingira asilia na kwamba ili ikae vizuri, iwekwe mwishoni mwa korido.

"Wall paper ya hifadhi za wanyama inafaa iwe na kundi la ina moja ya wanyama kama twiga au simba kulingana na mtu anavyopenda, uzuri wa wallpaper ni kwamba ni rahisi kuitoa pale unapohitaji kufanya hivyo wakati wowote," anasema.

Anashauri kuweka aina hizi za wallpaper kwenye ukuta mdogo na hasa kwenye kona ili kuongeza ukubwa wa eneo. Pia ni picha nzuri inayoweza kuwekwa upande wa pili wa kioo.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
WEWE! SAFARI YA WAPI WAKATI SIJAZIMA 'MZIKI'
MVUA
USIFIKIRI SIFA BABA!
MSAADA JAMANI KWANGU KUMEVAMIA NA MAJI...
WAHI POLISI KAWAAMBIE UMEVAMIWA
KWA KUWA USHAMWAMBIA MAMA YAKO KUWA TUNAPITIAGA SINZA NIKIKUFUATA SHULE SASA SIKUFUATI TENA SHOBO IKUISHE
BATHI AKINIFUATA MAMA NITAMPELEKA MPAKA KULEKULE KWA MAM'DOGO KILANGA KIKUISHE
WELEDI
'MWAKA MUPYA MAMBO MAPIYA 'MUSHAHARA YANGU INATOSHA' NAKAZA ROHO
KAMA KWELI MVUA ILIKUZUIA SIKU TATU USIRUDI MBONA JANA SIMU ILIPOKELEWA NA 'SAUTI YA KIKE?'
MKE WANGU TULIZAMALIZE 'KIBAHARIA'
JIRANI KUMBE ULIJUA NANUNUA BONDENI MBONA HUJANISHTUA?
MIMI NINGE-SHITULIWA UNADHANI NINGENUNUA HAPA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
HATA MTI UNAKATIKA LAKINI HAUNA KIUNO...

# Hali ya hofu yatanda mashariki ya kati

**SANAA, YEMEN**

HALI imekuwa ya wasiwasi katika eneo la Mashariki ya Kati baada ya nchi za Marekani na Uingereza kuishambulia Yemen kama hatua ya kulipa kisasi kutokana na waasi wa Houthi kuyumbisha usalama kwenye bahari ya Shamu.

Waasi hao wa Houthi walifanya mashambuzi kadhaa ya ndege zisizo na rubani dhidi ya meli za kibiashara zinazosafiri kwenye bahari hiyo kupinga jeshi la Israel kuendelea kuwaua wapalestina katika Ukanda wa Gaza.

Baada ya shambulizi hilo la Marekani na washirika wake, kundi la Houthi limeapa kulipiza kisasi baada ya ngome zao kupigwa kwa mabomu.

Uongozi wa waasi hao, umesema kitendo cha kushambuliwa kwa wapiganaji wake kama tukio la kihalifu na kuapa kuendelea kulenga meli zinazopita kwenye bahari hiyo kwenda nchini Israeli.

Aidha nchi ya Iran nayo imeapa kuendelea kusaidia waasi hao ambao wanawaunga mkono wapiganaji wa kundi la Hamas wanaopambana na jeshi la Israel.

Mashambulio hayo yalitekelezwa na ndege za kivita za Marekani na Uingereza, zililenga ngome 16 za waasi wa Houthi, ikiwemo ngome yake kuu na kuharibu silaha zake.

Rais Joe Biden alisema kitendo hicho kitasaidia, kulinda meli zinazotumia Bahari hiyo ili kuendeleza biashara za Kimataifa.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, alieleza ilikuwa jambo la muhimu kutekeleza mashambulizi hayo kwa ajili ya kujilinda.

Hata hivyo, Russia imelaani mashambulizi hayo, ikisema imekwenda kinyume cha sheria za Kimataifa, na kuishutumu Marekani na Uingereza kwa kutumia vibaya azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, lililotaka waasi wa Houthi kuacha kushambulia meli kwenye Bahari ya Shamu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres , ametoa wito kwa pande husika kupunguza mvutano katika Bahari ya Shamu, hali ambayo inaweza kuvuruga amani na utulivu wa kikanda. Msaidizi wa Katibu Mkuu kanda ya Mashariki ya Kati, Khaled Khiar, aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa kunashuhudiwa mzunguko wa ghasia ambao unahatarisha usalama wa kisiasa, athari za kiuchumi na kibinadamu Yemen na kanda nzima.

Balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa, Vasily Nebenzya, ameyataja mashambulizi hayo ya Marekani na Uingereza kuwa ni uchokozi wa silaha dhidi ya nchi nyingine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossein Amir-Abdollahian amesifu hatua za kundi la Houthi dhidi ya Israeli katika Bahari ya Shamu, na kuongeza kuwa Yemen imejitolea kuweka usalama wa baharini na meli zinazopita.

Kwenye chapisho lake katika mtandao wa X juzi, Amir-Abdollahian alisema kwamba hatua ya Yemen ya kuwaunga mkono wanawake na watoto wa Gaza na upinzani wake dhidi ya mauaji ya kimbari ya utawala wa Israel ni ya kupongezwa.


Pia aliitaka Marekani ikomeshe mara moja uungaji mkono wake kwa nchi ya Israel na kuanzisha mashambulizi dhidi ya Yemen ni kuhatarisha usalama katika eneo zima la mashariki ya Kati.

Taarifa kutoka mjini Gaza, zinaeleza usiku kucha wa jana Wapalestina walikabiliwa na mashambulizi ya mabomu kutoka vikosi vya Israeli.

Katika taarifa yake , wizara ya afya ya serikali inayoendeshwa na Hamas,ilisema kuwa watu 23,843 wameuawa huko tangu kuanza kwa vita hivyo Oktoba 7, mwaka jana.

Idadi hiyo ni ongezeko la watu 135,kulingana na idadi iliyotolewa Ijumaa ya wiki hii.

Wizara hiyo ilieleza watu wengine 60,317 wamejeruhiwa.



Mkazi wa eneo la Azhari mjini Khartoum nchini Sudan akikagua nyumba yake baada ya kuharibiwa na kombora jana. **PICHA: AFP**

# Watu 30 wauawa mapigano Sudan

KHARTOUM, Sudan

KUNDI la mawakili nchini Sudan wanaounga mkono demokrasia, limesema kuwa mapigano baina ya pande mbili zinazopingana yamewaua zaidi ya raia 30 kwa usiku wa juzi.

Walisema mashambulizi hayo yanayofanywa na wanajeshi kutoka kwa majenerali wawili yaliharibu makazi katika mji mkuu wa Khartoum.

Awali kundi hilo la mawakili lilisema katika taarifa yake kwamba watu 23 waliuawa siku moja kabla, na wengine kadhaa kujeruhiwa katika mashambulizi ya angani kwenye wilaya ya Soba.

Mawakili hao baadae waliongeza idadi ya watu 10 waliokufa katika mashambulizi mengine ya anga yaliyolenga maeneo tofauti.

Kundi jingine la kamati ya upinzani limeripoti raia wengine 10 kuawa kwa mizinga katika maeneo ya makazi na soko.

Mwakilishi wa Shirika la Kuwahudumia Watoto Duniani (UNICEF) nchini humo, Mandeep O'Brien, alisema kwamba vita hivyo vinaweza kusababisha janga kubwa kwa watoto milioni 24 wa nchi hiyo.

**DW**

## Cape Verde yatokomeza Malaria

**PRAIA,** CAPE VERDE

TAIFA la Cape Verde limekuwa nchi ya tatu kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria barani Afrika.

Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), kisiwa cha Cape Verde chenye watu 500,000, kinaungana na nchi za Mauritius iliyotokomeza Malaria mwaka 1973 na Algeria 2019.

Ili kutokomeza ugonjwa huo ambao unaendelea kuwaua maelfu ya watu barani Afrika hasa watoto wenye chini ya umri wa miaka mitano, nchi inapaswa kutoripoti kisa chochote cha maambukizi hayo kwa miaka mitatu mfululizo.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, alipongeza Cape Verde kwa kuushinda ugonjwa huo kutokana na mikakati yake ya kuimarisha sekta ya afya na kuwa mfano kwa mataifa mengine ya Afrika.

Duniani, ni mataifa 43 ambayo yamefanikiwa kuumaliza ugonjwa huo ambao mwaka 2022 pekee, ulisababisha vifo vya watu 608,000 na kuwaambukiza wengine milioni 250.

Malaria huambukizwa kwa kung'atwa na mbu wenye jinsia ya kike, wanaofahamika kwa jina la kitaalamu la Anopheles.

SAFU

MAKALA

# TUTUMIE NJIA ZA HAKI KUYAPATA MAFANIKIO



Na Magabilo Masambu

**Wengi waliofanikiwa kwa namna hii mwisho wao huwa si mzuri. Presha na sukari zinazowapata wengi zinatokana na msongo wa mawazo kwa sababu ndani ya mioyo yao wanafahamu maovu yaliyowapatia mali hizo. Tukifikiria kupata mali za haki uovu na uhalifu juu ya binadamu na wanyama utapungua sana.**

MAFANIKIO yoyote katika maisha ni mchakato mrefu. Jambo zuri tu ni kwamba tumepewa haki na nafasi sawa katika kuyatafuta mafanikio yenyewe, hivyo uamuzi unabaki kwetu ama tuyatafute au tusibiri kutazama wengine wakifanikiwa.

Mafanikio ya watu wengi mara nyingi yamekuwa ni siri kubwa. Wako wanaoonekana kufanya shughuli fulani lakini shughuli hiyo si ile iliyowapatia mafanikio hayo.

Si rahisi sana kwa wenye mafanikio makubwa kusema ukweli juu ya njia walizozitumia kuyafikia mafanikio hayo.

Kwa mfano, unaweza kumuona mtu ni kiongozi fulani na amefanikiwa sana ukadhani uongozi umempatia mafanikio, kumbe ndani yake kuna wizi wa mali za umma, rasilimali za nchi, uhujumu uchumi au aina nyingine yoyote ambayo si picha ya nje watu wanayoifahamu.

Wako watu wanafanikiwa kwa kuumiza wengine.

Wako wanaoteuliwa kwenye nafasi za madaraka kwa sababu wamewachongea wengine na kusababisha wafukuzwe kazi ili nafasi hizo zichukuliwe na wao.

Wako wanaoua ili wapate mali za marehemu, wengine wametuhumiwa kuua mpaka ndugu zao wa karibu ili wabaki na mali.

Wako wanaotuhumiwa na wengine kuthibitika kuua mpaka wenza wao baada ya kuona wamefanikiwa ili mali wabaki nazo. Wakati tunazungumza haya, wengine wanawaza kufanya hivyo sasa. Wengine wamedhulumu mali za wajane wamebaki wanahangaika ili wao wafanikiwe.

Hivi ni kweli damu za watu zimekuwa rahisi kuliko mali zao tunazochukua? Unajisikiaje kama wewe ni miongoni mwa waliotenda uovu huu ili ufanikiwe?

Ni ukweli kwamba mafanikio ya haki yanachukua muda mrefu, lakini ni bora ukachukua muda mrefu ukapata mafanikio yasiyo na majuto wala huzuni, huzuni na majuto huleta mfadhaiko wa moyo, yaani unakuwa na mali za kila namna lakini kila ukikumbuka namna ulivyozipata furaha ya moyo wako inajiondokea unabaki na furaha ya machoni tu ili kuwafanya watu wasigundue.

Wengi waliofanikiwa kwa namna hii mwisho wao huwa si mzuri. Presha na sukari zinazowapata wengi zinatokana na msongo wa mawazo kwa sababu ndani ya mioyo yao wanafahamu maovu yaliyowapatia mali hizo.

Tukifikiria kupata mali za haki uovu na uhalifu juu ya binadamu na wanyama utapungua sana.

Kama ni vyeo, tusubiri tuvipate kwa haki kwani kipimo unachotumia kumpimia mwenzako ndicho utakachopimiwa pia.

Kama ni polisi acha tabia ya kubambikiza watu kesi ili ufanikiwe haraka.

Utafanikiwa lakini utaandamwa na matatizo mengi katika maisha yako au ya ndugu zako kwa sababu wako watu mali wanazipata kwa jasho na damu halafu wewe unatumia mavazi ya umma kuwanyang'anya.

Kama ni daktari usiumize wagonjwa kwa kutaka upewe rushwa ndipo utoe huduma na kwamba kama rushwa haipo basi na kufa afe.

Akishakufa utajisikiaje maisha yako yote kila ukikumbuka kwamba ulikuwa sehemu ya kifo hicho? Kwa vyovyote damu hiyo itakulilia na hutabaki salama japo ni vigumu kujua namna malipo ya jambo hilo yatakavyokuwa.

Hali kadhalika kama hi hakimu, usifunge watu kwa sababu unakula rushwa ili ujenge mapema. Kwa kufanya hivyo unanunua maumivu ya kudumu bure.

Tusitumie nafasi zetu kuumiza watu ili tuyapate mafanikio kwa sababu ziko njia sahihi tu za kuyapata. Riziki ya mtu huwa haichukuliwi ila inaweza kuhifadhiwa kwa muda tu.

Nafasi kama si yako utaondolewa kwa kutumia njia zilezile ulizotumia kuwaondoa wengine. Ukitengeneza fitina utaondolewa kwa fitna vilevile kwani apandacho mtu ndicho avunacho. Ukipanda wema utavuna wema na ukipanda ubaya utavuna ubaya.

Kuna aina nyingine ya watu kazi yao kubwa ni kushiriki kukwamisha mafanikio na maendeleo ya wengine.

Hii inatokana na hofu ya kutojiamini. Kila unayemwona unahisi atachukua kazi yako au ataua biashara yako. Hofu hiyo huzaa uovu ambao unasababisha mpaka kuangamiza wengine ili kuendelea kulinda nafasi zao.

Hakuna raha yoyote ya kuwa na mali zenye huzuni na majuto. Kila mtu anayo kanuni ya maisha yake, hivyo usijilinganishe maisha yako na wengine japo unaweza kujifunza wanafanyaje.

Usitake mashindano ya maisha kwani hakuna aliyewahi kushinda kwa sababu kila mmoja ana wakati wake wa kufanikiwa.

Tatizo ni kwamba wanaoanza kazi leo wanajilinganisha na waliokaa katika kazi zaidi ya miaka 20. Usiendeshwe na hisia za wengine.

Ndoa nyingi zimeingia kwenye migogoro kutokana na kujilinganisha. Jirani yako anatoka na gari zuri asubuhi unaanza mbona wale wana nyumba, wana magari sisi kwa nini.

Je, wamekwambia wameyapataje? Ukiambiwa njia walizotumia utaziweza? Unataka uwe na mali huku ukiwa mwenye huzuni na majuto muda wote uko tayari?

Tukiacha kujilinganisha badala yake tukajifunza, basi tutapata mafanikio ya haki na yenye furaha japo yanaweza yasiwe makubwa bali yenye amani na Mungu atatubariki.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Ukimtaka msichana ongea vizuri, usimponde mwanaume mwenzio*



Na Adam Fungamwango

HIVI wewe nawe mwanamume gani yule wa kumkubali? Hana gari wala nyumba, atakupa nini? Hana mbele wala nyuma atakupa nini mtoto mzuri kama wewe? Mtu mwenyewe hajielewi yule, kapuku, hata kuvaa hajui. Umempendea nini yule? Kwanza hajasoma, kula yake yenyewe mchana ya shida, anashindia mihogo na chachandu, kweli mwanamke mzuri kama wewe uwe na mwanaume anayeshindia mihogo ya kukaanga kutwa nzima!?"

Ukitaka kujua kuwa kuna baadhi ya wanaume wanayatumia maneno haya kuponda wenzao, waulize wanawake. Wanawake siku zote ndiyo wanakutana na mauzauza ya wanaume ambao kila mmoja anakuwa na aina yake ya kupanga maneno kumvuta mwanamke.

Sasa ndiyo akutane na mtu wa aina hii ambaye hawezi kujieleza mpaka aponde wenzake ambao anaona kama na wao wanamzengea. Jamaa anayeponda wenzake anaendelea na kampeni yake ya kumtaka mwanamke, ameshamaliza kuponda sasa anaanza kujisifia mwenyewe.

"Nikubali mimi nina pesa, nimesoma, nina kila kitu ambacho wewe mtoto mzuri utahitaji, nitakufanya uwe malkia, mimi nina gari, nyumba na kila kitu ambacho mwanaume wa maana anatakiwa kuwa navyo, achana na hao wanaume nilivyovyoyaa, unajua shati hili nimenunua bei gani? Suruali, mkanda, sasa kuanzia leo hata wewe utaacha kuvaa mitumba wanaokununulia hao, utaanza kuva nguo za dukani."

Hii ni aina fulani ya utongozaji wa baadhi ya wanaume wanapowakabili wanawake, wakiwa na nia ya kuwashawishi wawe nao kimapenzi.

Kama mwanamke ambaye hitaji lake ni pesa za mkupuo anaweza kukubali, lakini ambaye anatafuta penzi hawezi kuwa na mtu kama huyo.

Ogopa sana mwanaume anayetafuta mpenzi kwa gia ya kuwa ana uwezo wa pesa kuliko wengine. Mara nyingi pesa hizo zinakuwa kwa muda mfupi, manyanyaso na masimango kwa sababu ndiyo hulka yake.

Mwanamke mwenye uwezo wa kufikiri vizuri hawezi kumkubali mwanaume anayeponda wanaume wenzake kwa sababu ya kasoro za kidunia na wala si za makusudi. Hawezi kumkubali kwa sababu ya uwezo wake wa kifedha kwa sababu ni za kwake na wala hazihusiani na yeye.

Kiasili mwanamke anamhitaji mwanamume ambaye hata kama hana pesa nyingi, uwezo, cheo wala elimu.

Anampenda na kumjali kwa dhati, anasikiliza na kumtimizia shida zake hizo hizo ndogo ndogo kila anapohitaji msaada.

Ndiyo maana hapa hatusemi kuwa pesa si kitu kwenye mapenzi, la hasha, pesa hurutubisha penzi, lakini isiwe ndiyo msingi wa penzi lenyewe. Ukitaka kujua hilo ni kwamba mwanamke anaweza kutoka kwa mwanaume mwenye uwezo mkubwa na kwenda kuishi na yule wa kawaida tu. Ni kwa sababu huku mwingine kuwa penzi la pesa la kitumwa, na sehemu nyingine hakuna pesa nyingi, lakini kuna mapenzi ya hiari, kujaliana, na kubembelezana.

Miaka ya 1980, mwanamuziki Cosmas Thobias Chidumule alitunga kibao kiitwacho, "Usitumie Pesa Kama Fimbo" ambacho kinazungumzia juu ya jamaa aliyekuwa na tabia kama hiyo. Chidumule ambaye kwa sasa ameokoka anapiga muziki wa Injili, alisema tukio hilo aliliona akiwa mkoani Arusha.

Kuna jamaa alikuwa amewaajiri kwenye bendi moja mtu na mpenzi wake, sasa wakati wa kulipa mshahara, alipoingia mwanamke, bosi akawa anamponda mfanyakazi wake wa kiume, akimtaka bibie kuachana naye awe naye yeye ambaye ni bosi, akiahidi kummalizia matatizo yake yote. Hata hivyo mwanaume alikuwa makini, ikashindikana.

Chidumule alisikia maneno yote kwa sababu alikuwa mlangoni, baada ya yule mwanamke ilikuwa ni zamu yake. Aliporejea Dar es Salaam kwenye bendi ya DDC Mlimani Park, akirejea kwa mara ya pili, akatunga kibao hicho chenye mashairi haya.

"Sikusimuliwa hayo ninayoyasema, nimekusikia wmenyewe ukimsimanga yule msichana.

Eti kwa nini amempenda kama Chidumule, kwanza fukara sina gari wala nyumba, nikampa nini ee huyo bibi jamani eee. Ameshasema hakutaki kaa chonjo, ameshasema hakutaki kaa chongo.

"Lazima katika mapenzi kamwe hakuna, na penzi la pesa duniani halipo, kwani hata kobe ana mpenzi wake na kamwe hajui pesa, ooo dada ninasema.

Unamponda kijana ili bibi akuthamini wewe, ukimpenda msichana sema naye polepole, kamwe hakuna haja ya kumkashifi kijana mwenzio oo baba.

"Usitumie pesa kama fimbo kaka, mambo ya pesa mpaka makubaliano, hapo ndipo pesa huwa na thamani ee. Ikiwa mapenzi mpaka bibi akupende, hata kama fundi wa kuhonga, lakini mpaka bibi akubali.

Ikiwa mapenzi mpaka bibi akupende, hata mzazi mwana lakini kwa mipango.

Cesi amesema Coasmas mpaka kufa ee, nami nasema Cesi wangu wa kufa na kuzikana oo, kipenzi changu mama.

Hata njia ana mpenzi wake kwenye tundu ee, ingawa njia hajui noti wala shilingi."

Haya wale madomo zege badala ya kutembeza sera mnaponda wenzenu mpo?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HIVI huyu mwanamke ana akili kweli? Kafundwa kwao?" Havijawa aliongea mwenyewe lakini kwa sauti. Halafu akazidisha sauti na kumwita wifi yake Sauda kwa ukali. "We mwanamke!" Sauda alikuwa ndiyo kwanza anatoka kuchota maji bombani ili mumewe akaoge, aende kazini.

Akamwita mumewe kwa sauti kuwa maji tayari aende akaoge. Alikuwa ameyaweka njiani kwenda bafuni. Yeye alikuwa anatoka tena na ndoo nyingine kwenda kuchota maji. Baada ya kusikia anamwita mumewe, huku mwenyewe akiwa anamwandalia mumewe maji, anasikia tena; " We mwanamke we! Hunisikii au!

"Unaniita mimi?" Akageuka.

"Nani sasa kama siyo wewe? Niko na nani humu ndani?"

"Wifi unaniitaje hivyo kama mtoto mdogo?" "Sina wifi kama wewe. Pu! Mungu anipushie, bado kabisaaa!" Akatema mate chini.

"Hivi wewe kwenu wapi? Na nashukuru kweli siku ya kuolewa sikuja, maana ningepoteza nguvu zangu bure."

"Kwani nimefanyaje?"

"Hivi haya ndiyo maji ya kumuwekea kaka yangu kwenye kuoga haya? Yaani meusiii kama lami halafu ya baridi. Mwanamke unapotoka kuchota maji, kwanza yakae yatulie. Haya si matope tu. Unataka kumuogesha kaka yangu matope!"

"Basi wifi...!"

"Basi wifi" Akamuiga huku akibana pua. "Hivi unajielewa wewe. Na sijui alikuokota wapi wewe. Ndiyo huko Kondoa!"

Maneno ya fedhuli na kejeli yalimkera Sauda. Akajikuta anashindwa kwenda bombani.

Akaweka ndoo chini na kuingia chumbani kwake. Akakaa kwenye kapeti na kuanza kulia.

Mumewe Kassim alikuwa amekaa kitandani. Aliyasikia maneno yote aliyoyasema dada yake. Hakuongea kitu chochote. Baada ya dakika tatu akatoka na kwenda kuichukua ndoo aliyoiweka mkewe na kwenda bafuni kuoga.

Hakutaka kumjibu chochote dada yake Havijawa. Alipomaliza kuoga alirejea ndani na kukumta mkewe akiwa ameshalia mpaka amechoka. Alibaki tu anatweta kama chura.

"Narudi kwetu." Maneno hayo machache yaliyotamkwa kwa sauti ndogo na dhaifu yalikwenda moja kwa moja kuchoma kwenye moyo ya Kassim.




**"Unajua na mimi naweza kuongea. Inawezekana zaidi kuliko yeye, mimi nakuheshimu wewe tu. Vinginevyo haniwezi kwa kubwata, hata nguvu za kunishinda mimi hana yule. naweza kumvuruga dada yako mpaka ukamwonea huruma!" Kassim hakujibu kitu, akawa anamwangalia mkewe kwa huruma.**

Kwake ilikuwa kama sauti kubwa ya radi iliyopiga kwenye moyo wake.

Mkewe kuondoka ni jambo ambalo hakutaka kabisa litokee maishani mwake. Sauda alikuwa kila kitu kwake.

"Hapana mke wangu, usifanye hivyo. Aliyekuoa hapa ni mmoja tu. Mimi si mwingine. Utaondoka mimi nikikuudhi na si yoyote yule."

"Hivi anayonifanyia dada yako ni sawa kweli? Nimeolewa na nani, wewe au yeye?" Akauliza Sauda kwa masikitiko huku akianza kububujikwa tena na machozi na akaanza kuyafuta yeye mwenyewe kwa kutumia kanga yake aliyovaa.

"Basi mke wangu, dada yangu ndivyo alivyo ndiyo maana ameshindwa kukaa na bwana amerudi tena hapa hapa nyumbani. Hawezi kukaa na mtu huyu. Kwa mdomo huu!"

"Unajua na mimi naweza kuongea. Inawezekana zaidi kuliko yeye, mimi nakuheshimu wewe tu. Vinginevyo haniwezi kwa kubwata, hata nguvu za kunishinda mimi hana yule. naweza kumvuruga dada yako mpaka ukamwonea huruma!" Kassim hakujibu kitu, akawa anamwangalia mkewe kwa huruma.

"Mwenzako hapa mimi hata sijielewi, sijui niende kwa dada yangu kwanza nikakae maana nimevurugwa hapa ujue..."

"Hapana mke wangu usifanye hivyo, usiende popote, mimi nipo upande wako, nitakulinda."

"Najua. Najua kuwa unanipenda sana mume wangu lakini inavyoonekana mtu anayeua ndoa yetu ni dada yako! Sisemi uende ukampige au umseme kwa ajili yangu lakini kuna kitu cha kufanya ili tuondokane na hii hali."

"Kitu gani mke wangu?"

"Ngoja nikifanyia kazi nitakwambia kesho!

**************************************

"Hodi hodi hodi." Ni sauti ya Havijawa ikiambatana kwa kugonga mlango kwa nguvu bila mpangilio wowote kwenye chumba cha kaka yake. Nia ni ile ile ya kumkorofisha wifi yake. Ni wakati ambao alijua kaka yake ameshaondoka kwemda kazini.

Siku hiyo aliondoka mapema sana. Havijawa anaona hii ndiyo fursa yenyewe.

"We bibi weweee, wanawake wenzio wooote wameamka umebaki wewe tu, jua la utosi wewe umelala, ndivyo ulivyofundishwa kwenu?"

Sauda baada ya kuona kero aliamka na kwenda kufungua mlango. Ile anafungua tu akakutana na jicho kali la husda.

"Enhee leo si zamu yako ya kufanya usafi, sasa mbona umelala mpaka saa hizi?" Baada ya jicho akasukumizwa na maneno.

"He wifi mbona nimeshafanya usafi?" "Usafi wa wapi wewe umefanya? Labda ulikwenda kufagia barabara huko njiani lakini siyo humu ndani.

Angalia uwanja mchafu, chooni kuchafu, bafuni kuchafu, halafu unasema umefagia, huko kwenu ndiyo huwa mnajifunza uongo hivyo?"

Ilionekana kabisa Sauda alipigwa na mshangao. Alisimama mlangoni kama jinamizi asiamini kile alichoambiwa. Anachokumbuka kwamba alikurupuka alfajiri kabla mumewe hajaamka, akaanza kufagia uwanja. Akaenda kufanya usafi bafuni na chooni, akamalizia na kupiga deki. Anashangaa kuona wifi yake anakuja kumwamsha na kumwambia hajafanya usafi wowote.

"Changamka bibi wewe, wenzako tunashindwa kwenda hata kuoga, bafuni kuchafu we umelala tu. Hapa umeolewa dada, hujaja kulala, kulala kwenu, siyo hapa..."

Wakati maneno yakimtoka Havijawa, Sauda aliamua kuwenda nje ili kwenda kuangalia maeneo yote ambayo anaambiwa hajafanya usafi. Kwanza kabisa ukumbini akakutana na michanga ambayo iligandamana na majimaji, ikionyesha kabisa kuwa ni kama hakukufanyika usafi wowote, au mpiga deki alimwaga michanga baada ya kufanya hivyo.

Akafungua mlango na geti la nje. Alichokutana nacho kilimshangaza. Uwanja ulikuwa na majani ya mti mkubwa uliokuwa kando ya nyumba hiyo. Alikutana na majani mengi makavu ambayo yalikuwa yamesambaa uwanja mzima kama vile hakukufagiliwa.

Kilichomshangaza zaidi ni kwamba si jambo la kawaida kwa muda wa alfajiri ambao alikuwa amefagia, majani mengi makavu yawe wameanguka tena kwa muda ule mfupi tu. Akaenda moja kwa moja hadi bafuni na kumalizia chooni. Kote alikuta kuchafu kama vile hakukufanyiwa usafi wowote.

Ilishamgaza, lakini akili yake ilikuwa timamu. Hakuwa kwenye ndoto alipoamka kufanya usafi. Akatoka tena nje na kwenda jalalani eneo ambalo alitupa majani makavu baada ya kuyafagia.

Alichofikiria kilikuwa sahihi. Wifi yake alikuwa nyuma ya yote hayo. Ni yeye ndiye aliyeacha wifi yake amalize usafi wote na kuanza kuchafua kwa makusudi.

Alianza bafuni na chooni. Akachota michanga na kumwagia ukumbini. Halafu akaenda kule alikomwaga majani makavu akayarudisha tena uwanjani, akayasambaza ili ionekane hakujafagiliwa kabla ya kwenda kumuasha mke wa kaka yake.

INAENDELEA JUMAPILI




# MAMA DANGOTE ATIBUA PENZI PEVU LA DIAMOND NA ZUCHU

MAMA mzazi wa mwanamuziki nyota wa bongo, Diamond Platnumz, Sanura Kassim maarufu kama Mama Dangote, amezidi kuongeza giza kwenye penzi la mwanawe na mwimbaji wa WCB, Zuchu.

Kulingana na kauli ya Mama Dangote, hajui kama Diamond ana uhusiano wa kimapenzi na Zuchu na kwamba anatambua msanii huyo yuko kama mwanamuziki wa WCB pekee.

"Hajawahi kuniletea Zuchu eti anataka kumuoa. Mimi najua Zuchu ni msanii wake," amesema Mama Dangote.

Mamake Diamond amesema kwamba mwanawe anaweza kuwa na uhusiano na wanawake hata mia moja, endapo hajamtambulisha na kumtolea mahari hatambui kama ni mwanamke wake halali.

# Hali bado tata kwa Kanye West


HALI inazidi kumwendea kombo rapa maarufu wa Marekani Kanye West, baada ya mwanaume mmoja kufungua mashtaka ya kumshambulia kimwili.

Mtandao wa TMZ, umeeleza mwanaume huyo ambaye ni shabiki yake alifanyiwa tukio hilo miaka miwili iliyopita.

Mwanamume huyo amedai licha ya kumuomba msamaha, mwimbaji huyo alizidi kumshambulia kwa kumpiga ngumi mfululizo.

Amedai kuwa mmoja wa watu walioandamana na Kanye alijaribu kuzuia shambulio hilo, lakini alimfokea na kumtaka aende nyumbani kwake akawachuke watoto.

"Kanye alipiga mayowe, nitakuonesha mfano mbaya, kisha alinipiga mimi ngumi usoni."amesema katika shtaka lake.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TODIBO ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United inatakiwa kulipa pauni milioni 52 ili kumnasa beki wa kati wa klabu ya Nice na timu ya Taifa ya Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 24.(***Caught Offside***)

### KUSI-ASARE ANYATIWA

MANCHESTER United pamoja na Chelsea wanavutiwa na mshambuliaji kinda wa Sweden, Jonah Kusi-Asare mwenye miaka 16 anayecheza katika klabu AIK. Bayern Munich pia wanavutiwa na kinda huyo. (***HITC***)

### BRUNO KUACHIWA

KLABU ya Newcastle wapo tayari kumuachia mwishoni mwa msimu kiungo wao kutoka Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26 kujiunga na Barcelona ama Real Madrid kwa dau la chini ya pauni milioni 100. (***Football Transfers***)

### HENDERSON ATAKIWA JUVE

KLABU ya Juventus imefanya mazungumzo na kiungo wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, juu ya uwezekano wa kumsajili kwa mkopo kutoka klabu ya Al-Ettifaq ya Saudia. (***Gianluca Di Marzio***)

### AJAX NAO WAMTAKA

KLABU ya Ajax ya Uholanzi nayo inasukuma kete zake kujaribu kumnasa Jordan Henderson ambaye anatarajiwa kufanya mazungumzo ya mustakabali wake na uongozi wa klabu yake. (***Standard***)

### NDOMBELE KUREJESHWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumrejesha kiungo wake, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 27 kutoka Galatasaray anapocheza kwa mkopo kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa kumnasa Conor Gallagher kutoka Chelsea. (***Football Transfers***)

### GOMES KUUZWA

KLABU ya Wolves italazimika kupewa kitita ili kumuuza kiungo wao raia wa Brazil, Joao Gomes mwenye umri wa miaka 22 katika dirisha la usajili la Januari. Tottenham Hotspur pia wanaripoti kuvutiwa na mchezaji huyo. (***Mirror***)

### TRAORE ATAKIWA

KLABU ya Klabu ya Napoli imetuma dau la usajili kwa kiungo wa klabu ya Bournemouth na timu ya taifa ya Ivory Coast, Hamed Traore mwenye umri wa miaka 23. (***Fabrizio Romano***)

### CLARKE ANYATIWA

WEST Ham na Crystal Palace wana nia ya kumsajili winga, Jack Clarke mwenye umri wa miaka 23 kutoka Sunderland, ambaye anakadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 20, huku klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur ikitarajiwa kupata asilimia 25 ya ada yoyote ya uhamisho (***Football London***)

### FOFONA AGOMBEWA

KLABU ya Burnley inatafuta mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 21, ambaye ameitwa kutoka kwa mkopo Union Berlin. (***Athletic***)

### LINGARD HATAKIWI TENA

KLABU ya West Ham haina nia ya kumsajili tena kiungo mshambuliaji wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 31, ambaye anapatikana kwa uhamisho wa bure. (***Standard***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KUIKOSA JANUARI YOTE

**MANHESTER,** England

●●● Anatarajiwa kuanza mazoezi kwenye kambi ya muda nchini Saudi Arabia...

ERLING Haaland anatarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi mwisho wa Januari, kocha wa Manchester City, Pep Guardiola amefichua.

Mshambuliaji huyo mahiri wa Norway amekosa mechi nane zilizopita za Man City, ikiwa ni pamoja na ushindi wa Kombe la Klabu bingwa ya Dunia nchini Saudi Arabia, kutokana na jeraha la mguu.

City walikuwa na matumaini ya kumkaribisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kurejea mapema mwaka mpya, lakini tatizo linaonekana kuwa la kutatanisha kuliko ilivyotarajiwa na bado hajarejea katika mazoezi kamili.

Matarajio sasa ni kwamba ataweza kurejea kazini huku bila mchezo wowote wikendi ijayo, wakati Klabu ikisafiri hadi Abu Dhabi kwa kambi ya mazoezi ya hali ya hewa ya joto baada ya mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Newcastle.

Guardiola alisema: "Ndiyo, amekuwa na matatizo kidogo ya kutatanisha katika miguu yake. Ni sawa lakini madaktari waliamua kusimama kwa wiki moja na labda kuanza tena kule Abu Dhabi.

> **"Natumaini mwishoni mwa mwezi huu atakuwa tayari. Ilikuwa zaidi kidogo kuliko tulivyotarajia mwanzoni.**

"Ni mfupa. Inahitaji muda. Kwa kila jeraha unaweza kufanya chochote unachotaka lakini ni suala la wakati."

Haaland alifunga mabao 52 msimu uliopita wakati wa kampeni bora ya kwanza akiwa na City na tayari alikuwa amefunga 19 msimu huu.

Aliongeza: "Tunamkumbuka sana Erling. Tunamuhitaji. Tunatumaini anaweza kurejea na kucheza.

"Unapojeruhiwa mwishoni mwa Novemba, unakosa michezo mingi. Ni kipindi kigumu zaidi."

Katika pigo zaidi kwa City, mlinzi Manuel Akanji anakabiliwa na kipindi cha kukaa nje ya uwanja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi alilazimika kutoka mapema katika ushindi wa Kombe la FA wikendi iliyopita dhidi ya Huddersfield.

Anaungana na beki wa kati John Stones kwenye orodha ya majeruhi.

Guardiola alisema: "Atakuwa nje kwa wiki kadhaa. Sio tatizo kubwa lakini hadi mwisho wa mwezi.

"Sasa tuna bahati kwamba hatuna mechi katika siku 10 zijazo baada ya Newcastle. Tutaona jinsi wanavyojisikia katika hali ya hewa nzuri huko Abu Dhabi."

# TEN HAG AMTUMIA SALAMU SANCHO



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amemtakia kila la kheri Jadon Sancho baada ya winga huyo kuondoka kwa mkopo Manchester United.

Sancho alijiunga tena na Borussia Dortmund kwa mkopo hadi mwisho wa msimu katika jaribio la kurudisha kiwango chake ambacho kimekwama tangu alipotofautiana na Ten Hag Septemba.

Baada ya kumtoa Sancho kwenye kikosi chake cha siku ya mechi kilichocheza na Arsenal, Ten Hag alitilia shaka viwango vya mazoezi vya winga huyo, lakini akapingwa na Sancho kwenye mitandao ya kijamii.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alidai kuwa alifanywa kuwa mbuzi wa kafara na kukataa kuomba msamaha kwa maoni yake kulimfanya akose kikosi cha kwanza.

"Natumaini anaendelea vyema, kwa hivyo namtakia kila la kheri," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni hivyo. Natumaini ataendelea vizuri na atafanikiwa."

Mkataba wa mkopo wa Sancho na Dortmund haujumuishi chaguo la uhamisho wa kudumu, huku mkurugenzi wa Dortmund, Sebastian Kehl akikiri wazi kuwa timu yake haiwezi kumudu kufanya hivyo.

Hata hivyo, Kehl aliongeza kuwa uhamisho wa kudumu unaweza kuangaliwa tena katika majira ya joto ikiwa mahitaji ya kifedha ya United yatakuwa ya kuridhisha.

Sancho atakuwa amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake atakaporejea Old Trafford, lakini United wana chaguo la kuongeza kwa miezi 12 zaidi.

United wana matumaini kwamba Sancho, ambaye alijiunga kwa pauni milioni 73 mwaka 2021, ataongeza thamani yake ya uhamisho huko Dortmund, ambapo alipachika mabao 50 na kusaidia mengine 64 katika mechi 137 kabla ya kuhamia Manchester.

## Pochettino ana wasiwasi na jeraha la Nkunku

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino amekiri kuwa na wasiwasi na jeraha la nyonga linalomsumbua kwa sasa fowadi, Christopher Nkunku.

Nkunku alikosa miezi minne ya kwanza ya msimu baada ya kupata jeraha la goti majira ya joto, na aliweza kucheza michezo minne tu kabla ya kupata jeraha la nyonga akiwa mazoezini ambalo limemfanya akose mechi mbili zilizopita.

Ripoti awali zilipendekeza suala la hivi punde la Nkunku lilikuwa dogo ambalo lingehitaji muda mfupi nje ya uwanja, lakini Mfaransa huyo bado hajarejea mazoezini na Pochettino amekiri kuwa hana uhakika ni nini kinaendelea na utimamu wa Nkunku.


"Nina wasiwasi kuhusu hali ya Nkunku," alikiri. "Nadhani ni siku kumi sasa hawezi kufanya mazoezi. Tunampima. Hatujui kitakachotokea. Nina wasiwasi kidogo kuhusu hali ya Nkunku.

"Nakumbuka mkutano wangu na waandishi wa habari baada ya hili kutokea. Lilikuwa suala dogo na gumu na imekuwa kati ya siku nane hadi kumi tangu alipofanya mazoezi.

Tulikuwa tukimsubiri kwa miezi sita na alikuwa karibu tena kujisikia vizuri. Alianza mchezo dhidi ya Palace na bila shaka alisikitishwa na hilo. Tunamtaka haraka iwezekanavyo kuhusika tena."



# PSG yajitosa kwa Kimmich



**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris St-Germain inapambana kuhakikisha inaipata saini ya kiungo wa Bayern Munich, Joshua Kimmich, katika dirisha hili kwa ajili ya kuboresha eneo lao la kiungo.

Kimmich mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akitajwa kuwa kwenye rada za timu nyingi kutokana na kiwango alichoonyesha na hali ya mkataba wake wa sasa ambao unamalizika mwaka 2025.

Hivyo Munich isipomuuza katika dirisha hili la uhamisho au mwisho wa msimu huenda ikamuuza kwa fedha kiduchu Januari mwakani ama akaondoka bure mwisho wa msimu ujao.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani huduma yake imekuwa ikiwindwa na timu nyingi Barani Ulaya ikiwa pamoja na Liverpool na Barcelona ingawa Munich ndio inaonekana kukwamisha dili lake kwani inahitaji zaidi ya pauni milioni 50.

Timu nyingi zinaona ni hasara kulipa kiasi hicho cha fedha kwa mchezaji ambaye mkataba wake unaenda kumalizika.

Hata hivyo, ushindani unaoongezeka kwa timu zinazomhitaji kuendelea kujitokeza, huenda ukasababisha timu mojawapo kulipa pesa hiyo inayotakiwa na Bayern na kumchukua fasta kutokana na kuhofia kupigwa bao na nyingine.

## HABARI MICHEZO

# LIGI KUU YATOA WACHEZAJI 19 AFCON

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imetoa jumla ya wachezaji 18 wanaochezea timu mbalimbali za taifa zinazoshiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) yaliyoanza jana nchini Ivory Coast.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, inaonyesha kuwa jumla ya wachezaji 14 wanaochezea timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars na waliobaki wanazichezea timu za mataifa mengine.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa Yanga ina jumla ya wachezaji saba kwenye timu mbalimbali kwenye Afcon, Simba ikiwa na wachezaji sita.

Simba na Yanga zote zina wachezaji wanne kwenye kikosi cha timu ya taifa, Taifa Stars, Azam ikiwa nao watatu.

Wakati Yanga ina wachezaji watatu wanaocheza timu za mataifa mengine, Simba ikiwa nao wawili.

Katika mchanganuo ni kwamba wachezaji wote wanaocheza Ligi Kuu walio kwenye Afcon, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Henock Inonga, Mudathir Yahaya, Mzamiru Yassin, Sospeter Bajana, Stephane Aziz Ki, Kibu Denis, Lusajo Mwaikenda, Kennedy Musonda, Djigui Diarra, Beno Kakolanya, Aishi Manula, Ibrahim Hamad 'Bacca', Bakari Mwamnyeto, Dickson Job, Feisal Salum, Clatous Chama na Abdulmalik Zacharia.

Wachezaji saba wa Yanga ni Mudathir, Bacca, Job, Bakari Mwamnyeto, ambao ni wanne wanaochezea Stars na Diara, Aziz Ki na Musonda wanaochezea mataifa mengine.

Diara yupo kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Mali, Musonda, Zambia na Aziz Ki, Burkina Faso.

Wa Simba ni Tshabalala, Mzamiru, Kibu na Aishi, hao ni wanne walio na kikosi cha Stars nchini Ivory Coast, huku wawili wanaocheza timu nyingine ni Chama wa timu ya taifa ya Zambia na Inonga wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Feisal, Lusajo na Bajana kutoka Azam, Kakolanya, Singida Fountain Gate na Zacharia wa Namungo FC.

## Ngoma sasa aandaliwa mkataba mpya Simba

INATOKA UK. 24

Ngoma, raia wa Jamhuri ya Kidemkrasi ya Congo aliichezea Raja Casablanca kuanzia 2019 hadi 2022 alipotimkia Al Fahaheel SC ya Kuwait, kabla ya kutua Al Hilal ya Sudan, lakini alivunja mkataba na timu hiyo mwaka jana kutokana na machafuko ya nchini humo kabla ya kutua Simba.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally amesema kwa sasa ambacho wanafikiria viongozi wa Simba ni kuimarisha kikosi na si kukibomoa.

"Nawahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa mchezaji yoyote ambaye yupo kwenye mipango ya mwalimu Benchika (Abdelhak) hatoondoka na timu imara inajengwa na kikosi imara, tuna ndoto zetu ambazo tumeziweka muda mrefu, hivyo ni lazima uwe na wachezaji wenye viwango vya juu na bora, hivi sasa tunaendelea kusaka wachezaji wenye ubora, siyo kuwauza. Siwezi kusema kama hili lipo, lakini mchezaji mzuri ambaye anahitajika hawezi kuondoka," alisema.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Imani Kajula ameeleza kufurahishwa na jinsi kikosi chao kinavyoimarika, hasa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

"Timu yenu inazidi kuimarika ikiwemo eneo la magolikipa, hivi sasa tuna chaguo pana sana kwenye upande huo, tuna Ayoub Lakred, Aishi Manula, Ally Salim, Hussein Abel, michuano hii imetusaidia sana kwa sababu tumetumia vijana wengi ambao huwa hawachezi mechi zingine hasa za ligi, kina Hussein Kazi wamecheza vizuri sana, tumemuona Israel Mwenda akicheza vema, michuano ya Kombe la Mapinduzi tumeitumia kwa ajili ya kujenga timu yetu, tunawapongeza wachezaji na benchi la ufundi, pamoja na mashabiki wa hapa Zanzibar, pamoja na waliotoka Bara kuja kutushangilia," alisema Ofisa huyo.



Vijana wakicheza Mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dodoma yafunga usajili na watatu

**Na Oliver Albert**

KOCHA mkuu wa Dodoma Jiji, Francis Baraza amesema ameongeza wachezaji watatu tu kwenye dirisha dogo la usajili.

Baraza ambaye pia aliwahi kuwa kocha wa Biashara United na Kagera Sugar alisema kikosi chake hakihitaji mabadiliko makubwa kwani bado kina wachezaji wazuri ambao wanaweza kuipa timu matokeo.

Alisema kabla ya usajili kufungwa ataongeza kikosini wachezaji watatu katika nafasi ya beki wa kati, kiungo na mshambuliaji.

Licha ya kwamba sina muda mrefu ndani ya timu hii lakini nimeona kikosi changu bado ni kizuri na hakihitaji mbadiliko makubwa kwa sasa.

"Jukumu langu kama kocha ni kuangalia sehemu yoyote iliyopo na mapungufu na kujaribu kuboresha sio kufukuza ndio maana nimeamua kusajili namba ndogo." Alisema Baraza.

Baraza alisema anaamini ligi itakapoanza watakuwa na mabadiliko makubwa kiuchezaji kwani sasa hivi wanafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika michezo iliyopita.

"Kusimama kwa ligi kutatusaidia kufanyia kazi makosa mbalimbali kwenye timu yetu na naamini ligi ikianza tutakuwa bora zaidi, "alisema Baraza

Dodoma Jiji iko nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 18 baada ya kucheza mechi 13, imeshinda tano, imetoka sare michezo mitatu na kupoteza mitano.

# Gamondi kuchukua maamuzi mazito Yanga

INATOKA UK. 24

benchi ambao walikuwa hawapati nafasi ya kucheza kwenye ligi Kuu na michuano ya kimataifa."

Aliongeza kuwa wako kwenye mapumziko mafupi na uongozi utafanya maamuzi mapema na kukamilisha usajili wa mwisho kwa nafasi aliyoipendekeza na kujulikana nani hatakuwa sehemu ya kikosi chao.



Alieleza kuwa wanatakiwa kufanya maboresho hayo madogo mapema kwa sababu wanaelekea mzunguko wa pili wa ligi hiyo ambayo itakuwa ya ushindani kwa kuwa timu nyingi zimefanya maboresho ya mapungufu yao.

"Hatutakuwa na maboresho makubwa, baada ya usajili tuliofanya wa Shekhan na Okrah, kuna mshambuliaji ambaye nilipendekeza na uongozi unafanyia kazi ili kuimarisha zaidi safu hiyo, kama itashindikana basi tutasubiri msimu ujao" alisema Kocha huyo ambaye anatumia likizo hii kuendelea kubaki Tanzania na familia yake kuhakikisha mambo ya timu yake yanaenda vizuri.

Michezo
Jumapili Januari 14, 2024
Nipashe



Haaland kuikosa Januari yote

UKU. 21

# Gamondi kuchukua uamuzi mzito Yanga SC

## ●●● Ni baada ya kufanya tathimini ya kikosi chake, asema malengo yametimia...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi ameanza kufuata maagizo ya uongozi kwa kufanya tathmini ya kikosi chake, kabla ya kuchukua maamuzi mazito ambayo yatatolewa hivi karibuni baada ya kufungwa dirisha dogo la usajili kesho.

Siku moja tu baada ya kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, Rais wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said alibainisha kuwa atapeleka mapendekezo kwa Kocha Mkuu, Gamondi kuondoa wachezaji ambao wameshindwa hata kuonyesha viwango katika michuano hiyo iliyofikia tamati jana.

Injinia alibainisha wazi kuwa Yanga haiwezi kukaa na mchezaji ambao ameshindwa hata kuonyesha uwezo kwenye michuano hiyo mifupi, achilia mbali Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika mashindano ya kombe la Mapinduzi Yanga iliondolewa katika hatua ya robo fainali, kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya APR ya Rwanda mchezo uliopigwa katika Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar.

Miguel alitumia mashindano hayo kuwapa nafasi ya kucheza wachezaji ambao hawakupata nafasi ya kucheza katika Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika na vijana wa U20 kwa ajili ya kutathimini viwango kabla ya kuchukua maamuzi ya kuwakata katika dirisha dogo.

Kupitia dirisha dogo la usajili Yanga imefanikiwa kukamilisha usajili wa mastaa wawili na kuwatangaza mpaka sasa ambao ni, Shekhani Ibrahim na kiungo wa kimataifa wa Ghana, Augustine Okrah huku wakieleza kuwa wapo katika hatua za mwisho za kushusha mshambuliaji wa kimataifa.

Yanga inatarajiwa kuachana na mshambuliaji, Hafiz Konkoni ambaye ameshindwa kupata nafasi na kushindwa kutimiza yale majukumu ambayo walitarajia kutendea haki nafasi ya Fiston Mayele.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema malengo ya kushiriki mashindano hayo, yametimia kwa kiwango kikubwa ya kwanza yalikuwa ni kuwatambua wachezaji wasiokuwa na sifa ya kubakia kuendelea Yanga.

Alisema ndani ya siku hizi mbili atakabidhi ripoti ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa uongozi na kufanya tathimini ya wachezaji, ikiwa ni siku chache tangu watoke kuondolewa katika mashindano hayo.

"Licha ya kuondolewa katika hatua ya Robo Fainali ya Kombe la Mapinduzi, lakini kwangu nimefurahia kuona malengo ya ushiriki wa mashindano haya kukamilika," alisema.

Yalikuwa ni mashindano ya kuwapa nafasi wachezaji wa

INAENDELEA UK. 23



Nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Fainali ya Kombe la Afrika (AFCON),dhidi ya Morocco itakayochezwa Januari 17, mwaka huu nchini Ivory Coast. PICHA: TFF

# Ngoma sasa aandaliwa mkataba mpya Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba ipo mbioni kumuongeza mkataba mwingine wa miaka miwili kiungo wake, Febrice Ngoma kwa ajili ya kuzuia jaribio la klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco inayoonesha nia ya kumhitaji.

Chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo kimesema kuwa tayari yameanza mazungumzo na mchezaji huyo ili kusaini mkataba wa miaka miwili kutokana na kuonesha kiwango cha hali ya juu kwa siku za hivi karibuni, ikiwemo kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kama kawaida, mchezaji akianza kuwaka Simba lazima zitokee timu zinaanza kuwanyemelea, Wydad Casablanca wameonesha kuwa wanamhitaji, walimuona katika mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika ambazo tumecheza nao, pia wanamfahamu kwa sababu alikuwa kule kule akicheza Ligi ya Morocco katika klabu pinzani ya Raja Casablanca," kilisema chanzo hicho.

Taarifa zinasema Wydad Casablanca walionyesha nia mara baada ya mechi ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa Desemba 19 mwaka jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 2-0.

"Naona jamaa wameonesha nia hasa kwa hiyo uongozi umeamua kufanya naye mazungumzo ili kumuongeza mkataba kwa sababu sasa hivi Simba imeshajifunza kuwa ukitaka kuwa na timu imara ni lazima ubaki na wachezaji wako tegemeo, kile kitendo cha kuwauza kirahisi Luis Miquissone kwenda Al Ahly (Misri), na Clatous Chama kwenda RS Berkane (Morocco) kimewafunza kitu kwa sababu baada ya pale timu iliyumba na haijakaa sawa mpaka sasa," chanzo kiliendelea kutoa taarifa.

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042